# Siasa ya Tanu katika Kilimo



SPE 5494
.5A7
S5

TWENDENI VIJIJINI

Kimeandikwa na

P. P. KIMITI

SOKOINE
NATIONAL
AGRICUTURAL
LIBRARY

# Siasa ya Tanu katika Kilimo

FOR REFERENCE ONLY

KIMEANDIKWA
NA
P.K.KIMITI

AFISA KILIMO/KATIBU MSAIDIZI
ELIMU YA SIASA (TANU)

7 OCT 2002

## YALIYOMO


UTANGULIZI — WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA

Sehemu ya Kwanza : — KAZI YA TANU KWA SASA

Sehemu ya Pili : — AZIMIO LA ARUSHA

Sehemu ya Tatu : — MISINGI YA SIASA YA UJAMAA

Sehemu ya Nne : — WIZARA YA KILIMO NA UTEKELEZAJI WA AZIMIO LA ARUSHA

Sehemu ya Tano : — MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO (WIZARA YA KILIMO)

Sehemu ya Sita : — SHABAHA NA MADHUMUNI YA VIJIJI VYA UJAMAA

Sehemu ya Saba : — UMUHIMU WA KUFANYA KAZI NA UTAMADUNI WAKE

# UTANGULIZI


TANU ya sasa ina kazi kubwa sana, maana TANU inafanya kazi ya kuelimisha, kueleza na kujenga Taifa letu ili litoke katika hali ya unyonge na kuwa katika hali ya neema na nguvu. Kama sote tunavyoelewa ni kwamba katika kuwaongoza wananchi, ni budi kwanza tuwasikilize, tushirikiane nao na tufanye kazi pamoja nao. Uhusiano uliopo kati ya Serikali na chama cha TANU ni mkubwa. Jambo la kukumbukwa ni kwamba chama siyo chombo cha Serikali, bali ni Serikali ambayo ndiyo chombo kinachotumiwa na chama katika kutekeleza matakwa yo yote ya wananchi ambao sisi sote tunawatumikia. Hii ndiyo maana tunasema kuwa chama kina wajibu mkubwa wa kufanya, katika kufikiria misingi ambayo baada ya kuwekwa kwa uwazi, ni budi Serikali ifuate na kutekeleza. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ni sehemu ya Serikali. Hivyo Wizara hii ina wajibu mkubwa sana katika kuitekeleza siasa ya TANU ambayo ndiyo inayoongoza Serikali.

Lakini hatuwezi kuitekeleza siasa hii iwapo hatuifahamu vizuri. Jitihada hii ya mwanzo ya kuelezea Msimamo wa Siasa ya Chama, ni mwangaza mzuri kwa watumishi wote, si kwa Wizara hii ya Kilimo tu, bali kwa watumishi wote wa Serikali. Ni tegemeo langu kuwa maandishi haya yatazidisha uelewano na ushirikiano mwema kati ya viongozi wote wa Wizara na TANU katika kuongoza na kuendeleza mbele uchumi wa Taifa letu; kwa manufaa ya wananchi wote kwa ujumla.

Tunayo kazi kubwa ya kufanya mbele yetu ya matatizo mengi ambayo yanawakabili wananchi wetu hasa huko Vijijini. Ni tegemeo langu kuwa tutashirikiana na wananchi vijijini katika kuitimiza mipango yetu tuliyoipanga. Kazi iliyobaki ni kusonga mbele na kwa juhudi kubwa katika kuutekeleza mpango huu wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; na hasa tukizingatia siasa ya kuimarisha Vijiji vya Ujamaa.

D. N. M. Bryceson,
Waziri wa Kilimo,
na Ushirika.

## SEHEMU YA KWANZA



**KAZI YA TANU KWA SASA**

TANU yaani Tanganyika African National Union, ni chama pekee cha siasa kilichomo Tanzania bara. TANU iliundwa tarehe 7/7/1954, baada ya kubadilisha chama cha kwanza kilichokuwapo yaani TAA (Tanganyika African Association) ambacho hakikuwa na madhumuni ya kugombea Uhuru, bali kilishughulikia shida mbali mbali za Waafrika katika matatizo waliyokumbana nayo katika maisha ya kikazi au starehe kwa ujumla. TANU ilipoundwa, ikabadili Katiba ya TAA na kuifuta kabisa TAA, ili TANU ambayo ilishika mahali pake, iweze kuwa na madhumuni ya kugombea UHURU wa Tanganyika. Tangu hapo TANU ikaanza shughuli za kisasa za kupigania Uhuru. Tangu hapo Mwalimu J. K. Nyerere alichaguliwa kushika kiti cha Urais wa chama.

**TANU YA ZAMANI**


Mara tu baada ya kuundwa kwa TANU, na kukubaliwa na Serikali kuwa chama cha siasa, TANU ilijishughulisha zaidi

na kuwapigia mayowe wakoloni ili waondoke na watuachie nchi yetu. Wakati huo mikutano ya hadhara yote, ilisikika mahali pote kwa kelele nyingi za "UHURU" "UHURU". Wananchi wengi, wake kwa waume vijana kwa wazee, walimiminika usiku na mchana katika Ofisi za TANU ili kwenda kujiunga na TANU. Wakati huo TANU ilikuwa ikithamini sana uwingi wa wanachama kuliko ubora wa wanachama wenyewe. Wakati huo, jambo hili la kuingiza tu wanachama bila kuwadadisi kama kweli ni Watanzania au vipi, halikuweza kufanyika, maana idadi kubwa ya wanachama ndiyo iliyosaidia kuihakikishia Serikali ya mkoloni kuwa kweli sisi Watanganyika, Na hivyo tukawaeleza watawala wa kigeni wa siku hizo kuwa dhumuni letu la kujiunga pamoja, ni kujitayarisha sisi wenyewe tulikuwa kwa pamoja tumejiunga katika kuidai haki yetu hiyo. kwa kujitawala. Ingawaje hatuwezi kukataa, sote tunaelewa wazi kuwa Serikali ya kikoloni ilijaribu kuweka kila aina ya vikwanzo licha ya kufunga baadhi ya matawi mengi ya TANU. Wananchi wengi walitiwa msukosuko, wengine walifungwa na zaidi ya yote, mikutano ya aina yoyote ile ambayo ilikuwa ikiendeshwa na TANU ilipigwa marufuku. Baadhi ya vibaraka wa wakoloni, walitumiwa ili kufanya fujo wakati wa mikutano ya TANU, ili mradi askari wajitie katika kuwatawanya kugundua ujanja wa wakoloni. Bila kukawia TANU iliamua kuanzisha jeshi lake la kuzuia fujo. Jeshi hilo la TANU la kuzuia fujo lilikuwa zaidi na vijana hodari ambao kweli walifaulu katika kazi yao. Huu ndiyo ulikuwa mwanzo wa "Vijana wa TANU" yaani TANU Youth League.

Maelezo hayo ni machache sana kwa kukupa mwangaza tu kidogo. Maelezo zaidi ya Historia ya TANU yanaweza kupatikana kutokana na vitabu vingi vilivyoandikwa na Makao Makuu ya TANU pamoja na baadhi ya wanachama wengi wa zamani. Vitabu kama "Ijue TANU" "Mkiki Mkiki wa Siasa Tanganyika" na "Mwito wa Uhuru" vyaweza kukupa kwa kirefu jinsi TANU ilivyoanza na matatizo yake yaliyoikabili kwa wakati huo. Tukiacha maelezo haya ya TANU ya tangu mwanzo, ebu tuangalie TANU ya SASA inafanya nini. Jambo hili ni la maana sana kwetu sisi kuelewa.

## KAZI YA TANU LEO

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzoni kuwa kazi ya TANU ya hapo awali kabla ya UHURU ilikuwa ni kuwapigia wakoloni



## KAZI YA TANU KWA SASA

TANU yaani Tanganyika African National Union, ni chama pekee cha siasa kilichomo Tanzania bara. TANU iliundwa tarehe 7/7/1954, baada ya kubadilisha chama cha kwanza kilichokuwapo yaani TAA (Tanganyika African Association) ambacho hakikuwa na madhumuni ya kugombea Uhuru, bali kilishughulikia shida mbali mbali za Waafrika katika matatizo waliyokumbana nayo katika maisha ya kikazi au starehe kwa ujumla. TANU ilipoundwa, ikabadili Katiba ya TAA na kuifuta kabisa TAA, ili TANU ambayo ilishika mahali pake, iweze kuwa na madhumuni ya kugombea UHURU wa Tanganyika. Tangu hapo TANU ikaanza shughuli za kisasa za kupigania Uhuru. Tangu hapo Mwalimu J. K. Nyerere alichaguliwa kushika kiti cha Urais wa chama.

## TANU YA ZAMANI

Mara tu baada ya kuundwa kwa TANU, na kukubaliwa na Serikali kuwa chama cha siasa, TANU ilijishughulisha zaidi

na kuwapigia mayowe wakoloni ili waondoke na watuachie nchi yetu. Wakati huo mikutano ya hadhara yote, ilisikika mahali pote kwa kelele nyingi za "UHURU" "UHURU". Wananchi wengi, wake kwa waume vijana kwa wazee, walimiminika usiku na mchana katika Ofisi za TANU ili kwenda kujiunga na TANU. Wakati huo TANU ilikuwa ikithamini sana uwingi wa wanachama kuliko ubora wa wanachama wenyewe. Wakati huo, jambo hili la kuingiza tu wanachama bila kuwadadisi kama kweli ni Watanzania au vipi, halikuweza kufanyika, maana idadi kubwa ya wanachama ndiyo iliyosaidia kuihakikishia Serikali ya mkoloni kuwa kweli sisi Watanganyika, Na hivyo tukawaeleza watawala wa kigeni wa siku hizo kuwa dhumuni letu la kujiunga pamoja, ni kujitayarisha sisi wenyewe tulikuwa kwa pamoja tumejiunga katika kuidai haki yetu hiyo. kwa kujitawala. Ingawaje hatuwezi kukataa, sote tunaelewa wazi kuwa Serikali ya kikoloni ilijaribu kuweka kila aina ya vikwanzo licha ya kufunga baadhi ya matawi mengi ya TANU. Wananchi wengi walitiwa msukosuko, wengine walifungwa na zaidi ya yote, mikutano ya aina yoyote ile ambayo ilikuwa ikiendeshwa na TANU ilipigwa marufuku. Baadhi ya vibaraka wa wakoloni, walitumiwa ili kufanya fujo wakati wa mikutano ya TANU, ili mradi askari wajitie katika kuwatawanya kugundua ujanja wa wakoloni. Bila kukawia TANU iliamua kuanzisha jeshi lake la kuzuia fujo. Jeshi hilo la TANU la kuzuia fujo lilikuwa zaidi na vijana hodari ambao kweli walifaulu katika kazi yao. Huu ndiyo ulikuwa mwanzo wa "Vijana wa TANU" yaani TANU Youth League.

Maelezo hayo ni machache sana kwa kukupa mwangaza tu kidogo. Maelezo zaidi ya Historia ya TANU yanaweza kupatikana kutokana na vitabu vingi vilivyoandikwa na Makao Makuu ya TANU pamoja na baadhi ya wanachama wengi wa zamani. Vitabu kama "Ijue TANU" "Mkiki Mkiki wa Siasa Tanganyika" na "Mwito wa Uhuru" vyaweza kukupa kwa kirefu jinsi TANU ilivyoanza na matatizo yake yaliyoikabili kwa wakati huo. Tukiacha maelezo haya ya TANU ya tangu mwanzo, ebu tuangalie TANU ya SASA inafanya nini. Jambo hili ni la maana sana kwetu sisi kuelewa.

## KAZI YA TANU LEO

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzoni kuwa kazi ya TANU ya hapo awali kabla ya UHURU ilikuwa ni kuwapigia wakoloni

mayowe na kudai UHURU. Ulikuwa ni wakati wa kumpigia mkoloni kelele tu, kumnyanyasa ili mradi kumtambulisha kuwa tulikuwa tumechoka kutawaliwa naye. Tulikuwa tukidai haki yetu ambayo kwa hakika baada ya kuona kuwa tulistahili kuwa nayo, mkoloni aliondoka na kutuachia nchi yetu ili tuiendeshe wenyewe. Ingawaje tuliwatukana wakoloni, ambao wanaweza kusema, walistahili matusi hayo, lakini katika TANU ya sasa, hatuwezi tena kufanya hivyo maana kazi ya kuendesha Serikali yetu tumeachiwa sisi wenyewe kama Taifa lililo huru la kujiamulia lifanye nini katika kujenga upya Taifa letu.

Kutokana na maelezo hayo, tunaona wazi wazi kabisa kuwa kazi ya TANU leo ni ngumu zaidi kuliko wakati ule tulipokuwa tukigombea UHURU.

Kama Mtukufu Rais wetu anavyoelezea kuwa kazi kubwa ya Chama cha siasa chenye nguvu, ni kuwa kiungo kinachowaungisha watu na Serikali walioichagua na kuwa kiungo kati ya Serikali na watu ambao inataka kuwatumikia. Hivyo tukirudi upande wa TANU, tunaona wazi kuwa TANU ina kazi ya kuwasaidia watu waelewe Serikali inafanya nini na kwa nini; pia ni budi kiwasaidie wananchi katika kuwaelekeza ili waweze kushirikiana na Serikali yao katika juhudi yao ya pamoja na kuondolea mbali *umaskini* ambao mpaka sasa umetuandama sana. Lakini pia TANU ya sasa ina kazi ya kuhakikisha kuwa Serikali daima inasikiliza na kuafiki mawazo, matatizo na matakwa ya watu. TANU ni msemaji wa watu. Licha ya hayo, chama hiki kinawaelemisha na kuwasaidia watu ili waelewe maana ya matendo fulani ya Serikali juu ya usalama wao wa baadaye na hali zao za baadaye. Kazi kubwa ni kujaribu kila njia ili kuelimisha, kueleza na kujenga taifa kwa kushirikiana pamoja. Jambo moja ambalo ni budi lijulikane na kueleweka ni kwamba CHAMA siyo chombo cha Serikali. Hii ina maana kuwa ni Serikali ambayo ndiyo chombo kinachotumiwa na chama katika kutekeleza matakwa ya watu na kuwatumikia. Kwa hiyo chama chetu cha TANU kina wajibu wa kufikiria misingi ya siasa ambayo Serikali yapaswa kufuata katika kufanya kazi zake.

Jambo la kukumbukwa pia katika uhusiano uliopo kati ya TANU na Serikali ni kwamba, TANU haiwezi kuchukua mahali pa Serikali; TANU haiwezi kufanya kazi ya kutunga sheria. Kwa kifupi ni kwamba TANU ya leo na hasa baada ya Azimio la Arusha, imeamua kwamba nchi yetu itajiendeleza katika

misingi ya kijamaa, yaani misingi ya kuishi bila kunyonyana. Hivyo kazi ya TANU ya leo tunaweza kuielezea kwa kifupi kuwa :

1. Kuelimisha na kutoa lengo la siasa yetu. TANU imekwisha tamka wazi msimamo wa siasa yetu ya Ujamaa na kujitegemea. Mtanzania wa kweli sasa inambidi afanye shughuli zake zote za maendeleo kwa kufuata siasa ya nchi hii yetu.
2. Kuwapanga wananchi katika utekelezaji wa Azimio la Arusha. TANU inawapanga wananchi kwa kuwashirikisha pamoja kufuata misingi ya Ujamaa. Vijiji vya Ujamaa, ni mfano mmojawapo wa kazi ya TANU. Pia katika mambo ya biashara na ulinzi wa Taifa.
3. Kuchunguza mazingara ya ndani na nje ya Taifa letu. Kuangalia maadui wa siasa yetu waliomo nchini na nje ya nchi. Licha ya kuchunguza maendeleo ya siasa yetu ili isiharibiwe na mtu yoyote, pia inawahimiza wananchi wawe macho kila wakati na maadui wa nchi yetu.
4. Chama kinasimamia utekelezaji wa siasa yetu. TANU husimamia kwa kupima mafanikio ya utekelezaji wa mipango iliyowekwa na kujaribu kila wakati kusawazisha matatizo yanayotokea.
5. TANU inatoa mfano bora wa uongozi wa kijamaa. Uongozi wa Chama unaambatana na mwenendo wa kidemokrasi ya Kijamaa, maana IMANI ya TANU inadhihirisha wazi kwamba HAKI na USAWA wa Binadamu ndiyo nguzo ya kuujenga Ujamaa.

### IMANI YA TANU

Siasa ya TANU ni kujenga nchi ya Ujamaa. Misingi ya Ujamaa imetajwa katika Katiba ya TANU, nayo ni hii :-

TANU inaamini kwamba :-

1. Binadamu wote ni sawa;
2. Kila mtu anastahili heshima;
3. Kila raia ni sehemu ya Taifa na anayo haki ya kushiriki sawa na wengine katika Serikali tangu ya Mitaa, ya Mikoa hadi Serikali Kuu.
4. Kila raia anayo haki ya Uhuru wa kutoa mawazo yake, wa kwenda anakotaka, kuamini dini anayotaka na kukutana na watu mradi havunji sheria.

5. Kila mtu anayo haki ya kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake na mali yake aliyo nayo kwa mujibu wa sheria.

6. Kila mtu anayo haki ya kupata malipo ya haki kutokana na kazi yake.

7. Raia wote kwa pamoja wanamiliki utajiri wa asili wa nchi hii ukiwa kama dhamana kwa vizazi vyao.


8. Ili kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi unakwenda sawa, Serikali lazima iwe na mamlaka kamili juu ya njia muhimu za kukuza uchumi; na

9. Ni wajibu wa Serikali ambayo ni watu wenyewe, kuingia kati kwa vitendo ya uchumi wa Taifa ili kuhakikisha ustawi wa Raia wote na kuzuia mtu kunyonya mtu mwingine au kikundi kimoja kunyonya kikundi kingine na kuzuia limbikizo la utajiri kufikia kiasi ambacho hakipatikani na siasa ya watu wote kuwa sawa.

Tumekwisha elewa kwamba Tanzania kwa hivi sasa inajenga Ujamaa. Lakini Ujamaa huu utajengeka tu iwapo wananchi wote, wake kwa waume, wataielewa TANU. Ni vigumu kwetu sisi kusema kuwa Serikali inaongozwa na TANU bila kuelewa TANU yenyewe. Tukiweza tu kuelewa TANU inafanya nini, basi mipango yetu yote ya maendeleo itaendeshwa moto moto kwa ushirikiano hasa wa watumishi wa Serikali pamoja na viongozi wote wa TANU. Tukiweza kuelewa uhusiano uliopo kati ya TANU na Serikali, hakika mafanikio yetu yataongezeka maradufu kuliko tulivyokuwa hapo mwanzoni. Mfanyakazi wa TANU au wa Serikali huwa ni mtu wa maana sana huko vijijini au mijini ikiwa tu, anafanya kazi zake barabara. Na zaidi ya hayo kama anafanya kazi pamoja na watu na akajipatia imani ya kuaminiwa, basi huwa kama mmoja wao ambaye huenda wakati wa shida, kutoa maoni au kuwaelezea jambo lolote la manufaa kwao. Hii ndiyo maana TANU inatukumbusha katika Azimio la Arusha kuwa "Twendeni Vijijini tuzungumze na wananchi kuona kama inawezekana au haiwezekani wananchi kuongeza juhudi."

## SEHEMU YA PILI

### AZIMIO LA ARUSHA



**Azimio la Arusha, liliungwa mkono popote nchini kwa vitendo.**

Kabla ya kuendelea na maelezo haya, ingefaa tuelezee :-

(a) Nini maana ya Azimio la Arusha ?

Kwa kifupi tunaweza kuelezea kuwa Azimio la Arusha ni TAMSHI rasmi la siasa ya chama chetu cha TANU ambalo linatoa mwongozo wa jinsi nchi yetu hii itakavyoendelezwa. Linaitwa "Azimio la Arusha" kwa kuwa lilipitishwa huko Arusha mwishoni mwa mwezi wa Januari mwaka 1967 na likatangazwa rasmi hadharani tarehe 5/2/67 mjini Dar es Salaam na Mtukufu Rais wa TANU Mwalimu Julius K. Nyerere.

(b) Jee Azimio hili lina sehemu kubwa ngapi ?

Katika kijitabu cha Azimio la Arusha ambacho kinapatikana katika lugha mbili; yaani Kiswahili na Kiingereza; zimo sehemu kubwa tano (5). Wananchi wengi bado wanadanganyika kwa kudhani kwamba Azimio la Arusha ni yale tu masharti

kwa viongozi, yaani kutokuwa na mishahara miwlii, kutokuwa na nyumba ya kupangisha au kutokuwa na hisa katika makampuni yoyote na kadhalika. Hii ni sehemu tu ya yale yaliyomo katika kitabu cha Azimio la Arusha.

Sehemu kubwa katika Azimio la Arusha ni pamoja na :-

1. SEHEMU YA KWANZA (Imani na Madhumuni ya TANU).
2. SEHEMU YA PILI (Siasa ya UJAMAA).
3. SEHEMU YA TATU (Siasa ya KUJITEGEMEA).
4. SEHEMU YA NNE (UANACHAMA).
5. SEHEMU YA TANO (Azimio la Arusha — Masharti kwa Viongozi).

Maelezo kwa kifupi :

(a) Sehemu ya KWANZA inatuelezea juu ya Imani na Madhumuni ya TANU.

(b) Sehemu ya PILI ambayo inaelezea siasa ya UJAMAA, inaelezea jinsi TANU inavyopinga unyonyaji; inavyopinga kuwepo kwa tabaka za watu yaani Mabwana na Watwana. Pia TANU inatujulisha kwamba iwapo tumeamua kufuata Ujamaa, basi Njia Kuu za Uchumi sharti ziwe chini ya wakulima na wafanya kazi (mfano, ardhi, mapori, misitu, njia za habari, njia za usafirishaji, viwanda, madini, mabenki, n.k.)

Zaidi ya hayo, Azimio linatukumbusha kuwa "Hapawezi kuwa na Ujamaa wa kweli bila ya Demokrasi. Hivyo ni budi Serikali ichaguliwe na kuongozwa na wakulima na wafanyakazi. Na mwisho Azimio linatuelezea kuwa "Ujamaa NI IMANI" na utajengwa na wanaoamini. Mwana TANU wa kweli sharti awe Mjamaa.

(c) Sehemu ya TATU inatuzungumzia juu ya siasa ya KUJITEGEMEA. Sehemu hii inatukumbusha jinsi unyonge wetu ulivyotufanya tuonewe, tunyonywe na tupuuzwe. Tunaji funza tokana na kifungu hiki kuwa MNYONGE hapigani na fedha maana fedha ni matokeo ya kazi siyo msingi wa maendeleo. Sehemu hii inazidi kusisitiza kuishi kwa kujitegemea kuliko kutegemea misaada na mikopo na hali tunajua wazi kwamba ipo hatari ya kuliangamiza taifa letu tukiendelea na mikopo. Mkazo zaidi umesisitizwa uweko vijijini, badala ya mijini peke yake. Masharti ya maendeleo yaani JUHUDI na

MAARIFA yameelezwa kwa kinaganaga katika sehemu hii. Maana tunaelewa wazi kwamba, hata tukiongeza juhudi kiasi gani, lakini bila ya kutumia maarifa, juhudi yetu inazaa matunda kidogo sana. Ujuzi hapa unatakiwa wa kujua namna ya kuongeza mazao yetu mara dufu.

(d) Sehemu ya NNE ambayo inazungumzia juu ya UANACHAMA inaeleza wazi kwamba TANU ni chama cha wakulima na wafanyakazi wote ambao wanakubaliana na Imani, madhumuni na sheria za TANU. Maelezo mengi jinsi ya kujiunga na chama pia yamo humo katika sehemu hii.

(e) Sehemu ya TANO ambayo ndiyo ya mwisho inaelezea juu ya masharti kwa viongozi. Hii ni miiko ambayo Kiongozi wa TANU na Serikali amekatazwa kuifanya. Miiko hii kwa kweli siyo kwa viongozi peke yao, bali kwa kila mwana-TANU halisi kuweza kuitekeleza. Viongozi wamepewa masharti hayo ili wao kwanza watoe mifano BORA kwa wananchi juu ya vitendo vyao na maisha yao pia. Hii itasaidia sana iwapo kiongozi atakuwa anaelezea ubaya wa kumnyonya mwenziwe — na huku yeye hakika hana mirija. Azimio la Arusha linasema kuwa "Wajibu wa kwanza wa mwana TANU na hasa kiongozi wa TANU, ni kutii kanuni hizi za Ujamaa hasa katika maisha yake mwenyewe. Kifungu cha (B) katika sehemu hiyo hiyo kinatuelezea kuhusu Serikali na vyombo vingine. Serikali inaagizwa ipange mipango maalumu kama ielezwavyo na tamko la TANU juu ya UJAMAA na KUJITEGEMEA. Kuna kifungu cha (c) ambacho kinaelezea zaidi juu ya uanachama kwamba ni budi wafundishwe kwa ukamilifu Imani ya TANU ili waielewe, na wakumbushwe wakati wote umuhimu wa kuishika Imani hiyo.

## MWISHO

Nadhani inaeleweka wazi kwamba IMANI ya TANU ni kujenga *UJAMAA* ambao ni mtindo wa maisha na msingi wake mkubwa ni Imani katika USAWA WA BINADAMU. Kwa hiyo huu ni mtindo ambao ni kinyume cha mitindo mingine iliyo na misingi ya unyonyaji. Mtindo huo wa maisha, unapinga kabisa na kutaka kutokomeza aina zozote zile za dhulma ya unyonyaji.

Siasa ya TANU (Policy) ni *Kujitegemea*. Kujitegemea kwa nchi kama hivi yetu kuna maanisha kuwa nchi hii itajiendeleza

kwa kutegemea raslimali yake, juhudi na uwezo wa wananchi wake bila kuombaomba misaada mingi toka nchi za kigeni. Msingi wake mkuu ni *kujiamini.*

## CHANZO CHA AZIMIO LA ARUSHA

Kwa nini Azimio la Arusha lilitokea ? Nini chanzo chake na kwa nini lilitokea mwaka 1967 na siyo kabla ya hapo (yaani mara tu baada ya Uhuru mwaka wa 1961) ?

Katika kuyajibu maswali haya ingefaa tuanze na swali la mwisho, yaani lile lisemalo kuwa, kwa nini Azimio lilitokea mwaka 1967 badala ya mara tu baada ya UHURU. Kwa kifupi tunaweza kulijibu swali hili katika sehemu kubwa mbili.


(a) Kuimarisha serikali yetu. Ilitubidi kufanya hivyo kwa sababu mara tu baada ya Uhuru Serikali yetu ilikuwa bado haijakamilika, maana tulikuwa bado tunao wageni wengi katika Serikali. Hivyo ilitubidi mpaka tuwapate wananchi katika kuishika Serikali vizuri. Wataalam wengi kwa wakati huo iliwabidi waendelee nasi ingawaje walikuwa wakoloni.

(b) Tulipitisha Azimio hili wakati huo, kwa sababu tulikuwa tumejifunza mengi kutokana na makosa yaliyotokea mara baada tu ya UHURU. Hii ndiyo sababu ya kusema kuwa "Chanzo cha Azimio la Arusha" ni kutokana na mambo matatu muhimu, ambayo tutayaelezea hapa chini.

Inaeleweka wazi kuwa, hapa petu Tanzania kuna wapinzani wa siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea. Wao wanasema eti Azimio la Arusha ni siasa ya kigeni ambayo Watanzania wameiga toka Mashariki. Mawazo ya namna hii tunayakataa na kuyaona kuwa hayana msingi wowote. Hii ni kwa sababu Azimio la Arusha limetokana na mambo matatu muhimu yafuatayo :-

1. *KATIBA YA TANU.* Katiba ya TANU tangu mwanzo imekuwa inasemea sana kuhusu Imani ya TANU. Kifungu cha kwanza kinaelezea "Usawa wa Binadamu." Vifungu namba sita, saba, nane na tisa vinaelezea juu ya Haki za Binadamu katika maisha yake. Haki ya Demokrasi na haki ya kumiliki mali ya umma kwa pamoja. Katiba ya TANU tangu mwanzo, ilithamini kuwepo kwa HAKI na UTU wa Binadamu kuweza kuhifadhiwa. TANU ilitambua kuwa ni wajibu wake kuendesha Taifa kutokana na Imani ambayo ilikuwapo tangu hapo mwanzo. Hivyo TANU haikuingiza jambo lolote geni katika

Katiba. "Nchi yetu ni nchi ya wakulima na wafanyakazi, lakini si nchi ya Ujamaa kamili. Tunaelezea hivi kwa sababu bado ina misingi ya ubepari na ukabaila pamoja na vishawishi vyake." Tusipoangalia misingi hii ya ubepari na ukabaila yaweza ikapanuka na kuenea. Maneno hayo yamo katika Azimio la Arusha na zaidi ya hayo, yamo maneno haya :- "Nchi yenye Ujamaa kamili ni nchi ya wafanyakazi, haina ubepari wala ukabaila : Haina tabaka mbili za watu; mtu hamnyonyi mtu mwingine, bali kila awezaye kufanya kazi hufanya kazi, na kila mfanya kazi hupata pato la haki kwa kazi aifanyayo na wala mapato ya wafanya kazi mbali mbali hayapitani mno." Kutokana na hayo, tunaona wazi kwamba hakuna tofauti kati ya maneno yaliyomo katika KATIBA ya TANU na yale yaliyomo katika Azimio la Arusha kuhusu usawa wa Binadamu.



2. Sababu ya pili ni "*HALI YA WANANCHI BAADA YA UHURU*. Jambo moja la kukumbukwa ni kwamba KATIBA ya TANU iliandikwa mwaka 1954 na mabadiliko yalifanyiwa mwaka 1962. Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo ni kwamba sababu kubwa zilizolifanya Azimio la Arusha kutokea mwaka

1967 ni mbili yaani ile ya kuweza *kwanza* kushika madaraka ya kisiasa, serikali, na tuwe na Uhuru kamili na hapo ndipo tuweze kukata mirija ya wanyonyaji. Iwapo tungefanya jambo hili kwa pupa, bila shaka matokeo yake yangekuwa kama yale yaliyotokea huko Kongo ambako mabepari au wakoloni walitumia hila za kumwua Waziri wa Kimapinduzi wa Kongo Patrice Lumumba eti kwa sababu alitaka kuipa nchi yake UHURU wa kweli kisiasa na kiuchumi. *Pili* ilitubidi tujifunze kutokana na makosa yetu wenyewe. Tukikumbuka wazi wazi kuwa wakati wa ukoloni tulilaumu wakoloni kwa mabaya yote yaliyotokea. Na tulikuwa na haki ya kufanya vile kwa sababu wakoloni waliwagawa watu wa nchi yetu katika makundi matatu :-

(a) Kundi la kwanza lilikuwa la wakoloni au Wazungu wenyewe. Wao walitunga amri zilizotawala siasa, uchumi na utamaduni. Sisi wananchi tulikuwa watwana wao.

(b) Kundi la pili lilikuwa la Waasia (Wahindi na Waarabu). Hawa hawakuwa na madaraka yoyote ya utawala, lakini waliweza kushirikiana na Wazungu katika kuwanyonya wananchi kiuchumi, kibiashara na katika baadhi ya viwanda. Kufuatana na hali yao, walipewa elimu nzuri pamoja na majumba mazuri kuliko yetu.

(c) Kundi la tatu lilikuwa la Waafrika. Hapa Waafrika walipewa jina jingine la dharau na kuitwa "NATIVES". Kwa ujumla Waafrika tulionewa, tukanyonywa na kupuuzwa katika kila hali ile. Maisha yalikuwa ya chini kabisa na daraja la Mwafrika likabaki "GRADE C". Hii ndiyo sababu ikatufanya tujiunge pamoja ili kudai na kupigania HAKI yetu kwa kutaka tupewe UHURU.

Katika mwaka wa 1961 baada ya kugombana na mkoloni, tukapata Uhuru. Hakika sote tulifurahi kwa kumwondoa Mkoloni lakini ingawaje tulijinyakulia UHURU wakati huo, kwa bahati mbaya sisi wenyewe tena tukashtukia tunajigawa katika makundi matatu makubwa; nayo ni :-

1. WATAALAM. Hawa walishika vyeo vyote vile walivyoacha wakoloni. Walipata mishahara mizuri, nyumba safi, magari na marupurupu mengine ya uhuru kwa sababu wao ndiyo waliokuwa na ujuzi.

2. WANASIASA. Hawa ni pamoja na viongozi wa TANU, Wabunge, Mawaziri na baadhi ya viongozi wa mashirika mbali

mbali ya Umma. Kundi hili lilipata nafasi ya kunufaika kutokana na vyeo walivyopewa na wananchi wenyewe. Hawa walianza kuotesha mirija mikubwa na kuanza kuwanyonya wananchi.

3. Kundi la tatu ambalo lilikuwa kubwa zaidi kuliko yote hayo mawili ya juu ni lile kundi la WAKULIMA NA WAFANYA-KAZI (Akina Baba Kabwela). Walijiona wamedanganywa sana maana matunda ya UHURU wao hawakuyapata. Wakazidi kunyonywa, mwisho ukafikia wakati wananchi wakawa wananung'unika.

Sababu ya tatu ya kuweko kwa Azimio la Arusha ni :-

3. UONGOZI BORA WA TANU. Hapa ingefaa ieleweke wazi kwamba watu waliopata nafasi ya kufaulu UHURU kuipata nafasi ya kunyonya ni hawa hawa viongozi wa TANU na Serikali. Wao walikuwa na madaraka ya majeshi, magereza, polisi nakadhalika. Wangeweza kujitungia sheria zozote zile za kuweza kuwanyamazisha wananchi ili wasizungumzie ubaya waufanyao viongozi. Lakini viongozi hawa hawa wa TANU walikubali kwa pamoja kukaa kitako na kufikiria matatizo ya wananchi. Waliazimia hivyo baada ya kutambua wazi kuwa walikuwa wanakwenda kinyume cha KATIBA ya TANU ambayo ilikuwa ya kujenga UJAMAA. Kutokana na mazungumzo na majadiliano kwa kirefu, ndipo wakaazimia kujirudi katika msingi wa Katiba yetu. Hivyo ukawepo umuhimu wa kuweka masharti (miko) maalum kwa viongozi. Azimio la Arusha sehemu ya TANO (5) inasema kuwa :-

1. Kiongozi wa TANU au wa Serikali sharti awe mkulima au mfanyakazi, na asishiriki katika jambo lolote la kibepari au kikabaila.
2. Asiwe na hisa katika makampuni ya kikabaila au kibepari.
3. Asiwe na mishahara miwili au zaidi.
4. Asiwe na nyumba ya kupangisha.
5. Asiwe mkurugenzi katika kampuni ya kikabaila au kibepari.

N.B. Viongozi tunaofikiria hapa ni :-

Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

Mawaziri.

Wabunge.

Wakuu wa vyama vilivyoshirikishwa na TANU.

Wakuu wa Mashirika ya Kiserikali.

Viongozi kutokana na kifungu chochote cha Katiba ya TANU.

Madiwani.

Watumishi wa Serikali wenye vyeo vya kati na juu.

Angalia : Kwa mujibu wa kifungu hiki, kiongozi ni mtu au mtu na mkewe au mke na mumewe.

**SERIKALI NA VYOMBO VINGINE**

Azimio la Arusha sehemu ya TANO kifungu cha (B) kinazungumzia kuwa TANU :

1. Inaipongeza Serikali kwa hatua zote ilizokwisha chukua mpaka hivi sasa katika kutimiza siasa ya Ujamaa.
2. Inahimiza Serikali, bila kungoja Tume ya Ujamaa, ichukue hatua zaidi za kutimiza siasa yetu ya Ujamaa kama ilivyoelezwa katika Tamko la TANU juu ya Ujamaa.
3. Inahimiza Serikali kutengeneza mipango yake kwa kutegemea uwezo wa nchi hii kuendesha mipango hiyo na wala isitegemee mno mikopo na misaada ya nchi za ng'ambo kama ilivyofanya katika mpango wa maendeleo ya miaka mitano. Halmashauri Kuu ya Taifa inaazimia mpango huo urekebishwe ili ulingane na siasa ya Kujitegemea.
4. Serikali ione kuwa mapato ya wafanyakazi nje ya Serikali hayapitani mno na yale ya wafanyakazi Serikalini.
5. Serikali itilie mkazo sana njia za kuinua maisha ya wakulima.
6. Inahimiza NUTA, Vyama vya Ushirika, TAPA, UWT, TYL, mashirika yoyote ya Serikali, kuchukua hatua ili kutekeleza siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Hayo yote ni mwongozo kwa Serikali katika utendaji wa mipango ya maendeleo. Serikali ni sisi wenyewe, ndiyo kusema kuwa tuna wajibu mkubwa katika kuyatekeleza yote hayo. Hatuwezi kuwaachia baadhi tu ya watumishi wa Serikali katika kutatua yote. Watumishi wote wa Serikali pamoja na wakulima na wafanyakazi ni budi tuungane bega kwa bega katika kuleta maendeleo. TANU iko daima pamoja nasi katika kazi zote za kulijenga taifa letu ambalo linaendelea tu kutokana na juhudi pamoja na maarifa yetu sote kwa pamoja.

# SEHEMU YA TATU

## MISINGI YA SIASA YA UJAMAA

Kutokana na Azimio la Arusha, Tanzania imeamua kujenga nchi ya Kijamaa.

Nini maana ya Ujamaa ?

Kwanza kabisa, ni budi tuelewe kuwa Ujamaa ni Imani ambayo katika Kiingereza inaitwa "Ideology". Huu ni mtindo wa maisha uliyo na mpango wa siasa na uchumi ambao unapinga kila wakati na kutaka kutokomeza kabisa aina yoyote ile ya unyonyaji. Pia unaondoa dhuluma zilizomo katika jumuia (Social injustice) ili kuhakikisha *usawa na haki za Binadamu*. Hii ndiyo maana TANU inasema kuwa haitoshi kuamini peke yake na kutoa hotuba nyingi majukwani kuhusu Ujamaa iwapo yule anayeuzungumzia, hautekelezi kwa vitendo. Ni budi utimizwe kwa ukamilifu katika maisha yetu ya kila siku. Tunakumbushwa katika Azimio la Arusha kuwa "Ujamaa ni Imani. Hauwezi kujijenga wenyewe. Utajengwa na wale wanaoamini na kuishi kwa mujibu wa siasa hiyo."

Misingi ya siasa ya Ujamaa imetajwa katika kitabu cha "Azimio la Arusha" na katika "Uhuru na Ujamaa". Misingi yenyewe ni :-




**Binadamu wa rangi zote huzaliwa na kukua sawa kabisa.**

1. Kule kukubali *USAWA WA BINADAMU* ndiyo nguzo ya msingi wa siasa ya Ujamaa. Mtu yoyote anayekataa usawa wa Binadamu, ni wazi kwamba hawezi kujiita Mjamaa. Kifungu cha kwanza katika Imani ya TANU kinasema kuwa *"Binadamu wote ni sawa."* Kukubali usawa wa Binadamu ndiko kunako tekeleza usawa huo kwa vitendo na kufanya heshima ya kibinadamu, upendo wa kidugu pamoja na kuwepo kwa ushirikiano bora miongoni mwa Jumuia ya Binadamu. Tuzungumzapo kuhusu Usawa wa Binadamu, hatuna maana ya ukubwa, unene, urefu au mapato. La hasha, hapa mkazo unatiwa kati neno *"UTU"*. Uwezo na mahitaji ya lazima kwa Binadamu ni budi vitiwe maanani. Mfano kila binadamu wa rangi yoyote ile, huzaliwa, kukua na hadi kufa sawa kabisa. Mahitaji ya lazima kama :-

(i) Chakula;
(ii) Mavazi na
(iii) Malazi.

Ni vya muhimu sana, na ili binadamu aweze kuishi katika hali ya ubinadamu, ni lazima apate hivyo vyote. Heshima, cheo au madaraka au akili ya mtu, haimfanyi mmoja asiweze kuitwa Binadamu. Maelezo haya ni kwa kifupi, na ni tegemeo letu kuwa maelezo haya yatatoa mwangaza kidogo kwa wasomaji.



**Njia kuu za uchumi sharti zimilikiwe na wakulima na wafanyakazi.**

2. Umilikaji na Utawala wa pamoja Njia kuu za Uchumi.

Kwa kuwa TANU inaamini kuwa Binadamu wote ni sawa, hivyo ni budi Njia Kuu za kuzalisha mali. ni lazima zimilikiwe na wananchi wote. wa jumuia ya wote wale wanaohusika. Mfano Watanzania, ni budi kwa pamoja wazimiliki njia hizo. Hii itakomesha limbikizo la mali kwa watu wachache ambao hawana haki hiyo.

3. Kazi ni Msingi wa Maisha ya Binadamu.

Kwa kuwa kazi ni msingi wa maisha ya Binadamu, hivyo ni haki na ni wajibu wa kila mtu kufanya kazi. Hatuwezi kuinua maisha yetu, lau kama njia Kuu zote za kuzalisha mali zinamilikiwa na wananchi, iwapo hatufanyi kazi. Kama tunataka maendeleo zaidi. hatuna budi tufanye kazi zaidi.

Vitu vyote duniani ni matokeo ya kazi. Hata binadamu mwenyewe ni matokeo ya kazi ya Mungu. Hii ndiyo maana kila mtu inambidi afanye kazi kwa uwezo wake wote na apate pato la haki kutokana na kazi yake. **(bila kunyonywa)** au kumnyonya mwingine. Tutafanikiwa katika lengo hili la kutonyonywa, iwapo tu kila mtu atafanya kazi. Makundi (tabaka) mbili yaani za wafanyakazi na wafanyiwa kazi zitatoweka kabisa.

4. Mpango wa Uchumi na Maendeleo.

Nchi au Taifa linalojenga Ujamaa. halina budi kuhakikisha kwamba kuna Mipango maalum ya maendeleo. Mipango hii ni budi ihusiane na mambo haya:—

(i) Kuchagua kwanza mambo muhimu ya kuanza (Priorities).

(ii) Kuweka shabaha maalumu (targets).

(iii) Kupima mafanikio.

5. Demokrasi:

Nchi inayojenga Ujamaa haina budi kuhakikisha kwamba kuna Demokrasi kamili ili kuhakikisha kwamba matunda ya jasho la wakulima na wafanyakazi, yanatumika kwa manufaa ya Umma; maana hasa ya Demokrasi ni (utawala wa watu). Demokrasi iliyokamili ni budi iwe na haya:—

(i) Uwezo wa kuchagua na kuondoa viongozi wao wenyewe.

(ii) Kushiriki kwa ukamilifu katika kuamua na kupendekeza shughuli zinazohusu maendeleo yao.

(iii) Uongozi wa pamoja katika kuamua na pia kuwa na madaraka binafsi katika kuamua na kutekeleza.


## CHAMA NA UJAMAA

Ili Ujamaa uweze kufanikiwa ni lazima mambo haya yafuatwe na kutekelezwa; TANU inafuata nguzo zile za lazima katika kuijenga UJAMAA. Hii ndiyo maana Chama chetu kitukufu kinaona umuhimu wa mambo haya yafuatayo :

1. Chama kinachotawala ni lazima kiwe cha kijamaa. Maana hatutegemei kuona chama cha siasa cha kikabaila au cha kibepari kinajenga Ujamaa. Huu utakuwa muugiza mkubwa iwapo jambo hilo litatokea.

2. Uongozi wa chama ni budi uwe wa Kijamaa. Viongozi hawa ni budi wao wenyewe wawe wakulima au wafanyakazi. Itakuwa kinyume iwapo viongozi wa chama watakuwa mabepari au makabaila na huku tukasema ni viongozi wa chama cha Ujamaa.

3. Siasa ya chama ni budi iwe wazi na ya kueleweka na kila mtu katika umma ili lengo lake liweze kujulikana wazi bila ya mafumbo.



**Wananchi wanao uwezo wa kuchagua na kuondoa viongozi wao.**

4. Chama ndicho kiwe na kauli ya mwisho katika mambo ya siasa ya nchi. Hii huitwa kwa Kiingereza 'supremacy' ya Chama.

## SEHEMU YA NNE

## WIZARA YA KILIMO NA UTEKELEZAJI WA AZIMIO LA ARUSHA

Mtukufu Rais Mwalimu J. K. Nyerere ameelezea mara nyingi na hasa katika kitabu cha "Utekelezaji wa Azimio la Arusha" kuwa "Kukubali Azimio la Arusha ni sawa na kijana wa Kikristo kupata kipa-Imara, au kijana wa Kiislamu kusilimishwa." Ingawaje nchi yetu haijawa ya Kijamaa kamili lakini ni wazi kwamba tumo mbioni katika kuujenga Ujamaa. Ieleweke wazi kwamba, hatuwezi kuukamilisha Ujamaa wetu iwapo hatujitegemei. Ndiyo maana siasa yetu inaitwa ya "Ujamaa na Kujitegemea." Wengi wetu tumejaribu na kufanya vitendo tukifikiria kuwa kujitegemea maana yake ni kujitosheleza kwa wataalamu na fedha. Hii siyo maana yake hasa. Maana yake kubwa ni kwamba :—

(a) Hatuna budi kutumia kwa juhudi zetu zote raslimali yetu tuliyonayo.

(b) Raia wapewe nafasi katika kila kazi mara wanapoonekana wanajimudu katika kufanya kazi hiyo barabara.

Katika sehemu ya fedha, Azimio la Arusha linatueleza kuwa hatutakataa misaada; ila linasisitiza kuwa "kundi moja tu la watu tutakaowategemea ni sisi wenyewe; hatutaendesha nchi yetu au maisha yetu katika hali ambayo tutashindwa kupata maendeleo yoyote bila fedha kutoka nchi za nje." Hii ndiyo maana mpaka sasa tumekubali kupokea baadhi tu ya misaada ambayo haina masharti ya kuliangamiza Taifa letu lililo huru. Lakini tangu sasa, Azimio la Arusha linatuambia, tutasimama wima na kutembea kwa miguu yetu badala ya kupinduka na kuwa miguu juu vichwa chini. Viwanda vitakuja, na fedha zitakuja, lakini msingi wake ni **Wananchi** na **Juhudi** yao na hasa katika **KILIMO.** Hivyo ili tuweze kufikia lengo letu, ni budi tulete **Mapinduzi katika Kilimo.**

Tumeamua kuishi kijamaa kwa namna ya usawa wa kidugu. Tumeamua kufanya kazi pamoja kwa faida ya wote.

Hii ina maana kubwa, kwa sababu sehemu kubwa ya kilimo chetu itafanywa na makundi ya wananchi wanaoishi pamoja na kufanya kazi kidugu. Ni wazi kwamba iwapo tutafanya kazi pamoja tutaweza kuongeza mapato yetu na kuleta manufaa zaidi kwa kila mtu. Ili tuweze kufanikiwa katika lengo hili, ni budi watumishi wa Kilimo wote kwa pamoja walete mapinduzi haya, na kufanya kazi kwa bidii zaidi na kwa maarifa zaidi. Sote tunatambua wazi kuwa nchi yetu ina bahati kubwa ya kuzawadiwa ardhi nzuri na kubwa kuliko nchi nyingine ambako watu wako tayari kulima sana, lakini wanakosa ardhi. Sisi tumezawadiwa nafasi hii, hivyo ni lazima tuwaendee wakulima vijijini ili tusaidiane nao katika kuifanya ardhi hii itupatie mahitaji yetu.

Azimio la Arusha linatuelezea kuwa "Ardhi ni ufunguo wa maisha ya binadamu, kwa hiyo Watanzania wote waitumie ardhi kama ni raslimali yao kwa maendeleo ya baadaye." Iwapo tunakubaliana sote pia kuwa "Fedha ni matokeo siyo msingi wa maendeleo" na kwamba nchi yetu bado ni maskini; hivyo ni wazi ya kwamba maendeleo yetu yataletwa na Kilimo. Ardhi



**Tuishi pamoja, tufanye kazi pamoja kwa faida ya wote.**

nzuri tunayo, ambayo inaweza kutoa mazao mengi ya chakula .....kwa ajili ya fedha. Nchi yetu pia ni nzuri kwa ufugaji na uvuaji wa samaki. Iliyobaki ni sisi kwenda vijijini na kuzungumza na wananchi, jinsi wawezavyo kuongeza Uchumi wa Taifa.

Katika kuleta mapinduzi ya Kilimo huko vijijini, ni lazima na inafaa ikumbukwe kuwa lengo letu kubwa ni la vijiji vya Ujamaa ambalo litaleta maendeleo na kujenga Taifa lenye nguvu. Hali kadhalika ni lengo la UONGOZI BORA huko vijijini. Mabwana Shamba huko vijijini, ni lazima watambue wajibu wao mkubwa. Ni budi watambue shida kubwa za wakulima wetu. Hivyo kazi kubwa ya Bwana Shamba ama kiongozi yoyote, ni ile ya kushirikiana na wananchi pamoja katika kuyaleta maendeleo yetu wote kwa faida ya wote. Kitu kilicho muhimu hapa ni wale watu wenyewe na jinsi viongozi hawa wawezavyo kwenda nao bega kwa bega katika shughuli zote hizi za uchumi. Mabwana shamba ni lazima wawe na *fikara za Kimapinduzi*. Ni lazima waache uongozi wa nyakati za zamani; na lazima watambue umuhimu wa kushirikiana katika kazi zote huko vijijini kwa maendeleo ya watu. Tusipende chuki ya zamani iliyo kuwepo kati ya Bwana Shamba na mkulima iendelee. Tukae chini pamoja nao ili tuelezane kwa kirefu jinsi tutakavyo kuza kilimo chetu nchini. Ili tuweze kufanikiwa katika lengo letu hili la uongozi bora vijijini ni budi :

1. Tuwaendee watu.
2. Tuishi pamoja nao.
3. Tujifunze kutoka kwao.
4. Tufanye mipango yetu pamoja nao.
5. Tuanzie kwa mambo wanayoyafahamu.
6. Tuwapende.
7. Tuwafundishe kwa vielelezo na vitendo.
8. Tuwafundishe vitu, hatua kwa hatua na mwishowe tuwafanye waweze kujitegemea wenyewe.

Kabla hatujaendelea na maelezo mengine kuhusu hasa mpango wa Wizara katika miaka mitano, tungependa kukumbusha kuwa kosa kubwa tulioachiwa na mkoloni la wakulima wetu kukimbilia kulima mazao ya fedha tu, ni budi tulipige vita. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Bwana

D. Bryceson alipokuwa akihutubia vijana mjini Dar es Salaam tarehe 2/2/69, alisema kuwa : sababu ya kubadilisha na kuongeza neno "chakula" katika Wizara ilikuwa kwa ajili ya "kujaribu kufikiria kwa makini juu ya *umuhimu wa chakula bora*. Tumekuwa tukizungumzia juu ya umashuhuri wa chakula bora kwa muda mrefu sana, lakini mara nyingi *maafisa wetu wa Kilimo* mashambani wamesahau kutilia mkazo juu ya jambo hili dogo, lakini muhimu. Hasa kwa wakulima wanaofanya kazi kwa bidii, chakula bora ni lazima kwao ili kuwawezesha kufanya kazi nzuri ya kutosha kila siku katika mashamba yao." Maelezo haya yamedhihirishwa na wataalamu popote duniani, kuwa mtu au binadamu yoyote anayekula vizuri, huweza kufanya kazi yake vizuri (kwa kutumia akili na musulu wake pia). Hivyo katika siasa yetu na hasa kwa upande wa Kilimo, shabaha yetu ni :-

(a) Kuwapatia wananchi chakula cha kutosha na kilicho bora.

(b) Kulisha viwanda vyetu wenyewe kwa kutoa mazao mengi.

(c) Kuuza mazao ya kutengenezea vitu mbali mbali kwenye viwanda vya nchi mbali mbali.

Umuhimu wa kutilia mkazo chakula kwa sasa umeanza kueleweka na wengi. Mazao ya fedha bado hayajawa na matatizo makubwa licha ya kupata masoko ya kutosha. Lakini tatizo hili litapungua kadri tutakavyokuwa tunaendelea katika upanuaji wa viwanda vyetu.

Ukulima wetu ni budi uundwe upya katika njia ambazo mazao bora zaidi yataweza kupatikana kwa wote walio radhi kutoa jasho lao, na kwamba maisha yetu huko vijijini ni budi yawe ya Ujamaa, yaani ya kuweza kufuatana na misingi ya *Usawa, ushirikiano* na *demokrasi*. Wataalamu wa Kilimo, ni budi wajitolee kwa Taifa lao hasa kwa upande wao na kuongoza kilimo bora. Wafanye kazi kama raia walio sawa na waifanye kazi hiyo kwa faida ya wote. Ni budi sote kwa pamoja — tutambue kuwa tunayo kazi kubwa ya kufanya kabla ya kuwa na haki ya kujivunia mafanikio yetu. Maisha yetu sote (wakulima na wafanyakazi) yatakuwa mazuri tukifanya kazi. Kazi hizo tuzifanyie kule kule kunakohitajika kufanyiwa kazi. Wataalamu wote wa kilimo ni budi tuelekeze utaalamu wetu huko vijijini ambako ndiko wakulima waliko. *Sote kwa pamoja, viongozi wa TANU na Serikali, wakulima, wataalam, wanafunzi na kila mtu, sasa tuamue kwamba kuanzia sasa tutafanya kazi kwa bidii, kwa akili, na kwa faida yetu na watoto wetu.*

# SEHEMU YA TANO

## MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO (1969 - 1974)

Mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano unatuelezea jinsi Serikali yetu itakavyoendelea katika kutekeleza mipango ambayo inaambatana na siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea. Kama sote tuelewavyo ni kuwa nchi yetu bado maskini, lakini hata hivyo yapo mahitaji makubwa kwa ajili ya maendeleo. Matatizo yote kuhusu umuhimu wa kujiendeleza unaonekana dhahiri kutokana na wilaya zetu, kazini mwetu na hata katika jamii zetu. Serikali inajitahidi sana kuitumai raslimali hii kidogo tuliyonayo kwa kupata maendeleo haya makubwa. Katika mpango huu, hakuna sehemu itakayo sahauliwa, hata hivyo ni budi tutambue kuwa hatuna fedha za kutosha katika kumridhisha kila mmoja wetu. Hivyo ulingano ni budi uwekwe kati ya mahitaji yote hayo.

Mpango huu, unamhusu kila mtu, na kila Wizara; maana maendeleo hayawezi kufanikiwa ikiwa kila mmoja wetu atafanya lwake. Mfano, maendeleo yetu yametiliwa mkazo yafike huko vijijini. Bwana shamba au Wizara, itashughulikia sana, na ukuzaji na uuzaji wa mazao. Lakini mazao lazima yasafirishwe, hivyo Idara ya kazi inahusika sana na kutengeneza barabara; na kadhalika.

Katika mpango wa kwanza yaani wa tangu 1964 - 1969 mafanikio yake yalikuwa mazuri. Wananchi popote pale walijitahidi sana katika kuutekeleza mpango huo, na hasa mara tu baada ya Azimio la Arusha, kazi mbali mbali za maendeleo kwa kujitolea zimeendeshwa vizuri sana nchini.

Lakini pia ingefaa tuangalie kama mipango hii hutengenezwa namna gani. Ni hatua zipi mpango kabla ya kupitishwa, ni budi upitie. Hatua hizi ambazo ni kwa kifupi, zitakusaidia kutambua jinsi mpango ulivyoendeshwa; kufuatana na mahitaji ya umma.

1. Wizara mbali mbali zilitayarisha mipango yao zikishirikiana na watumishi toka Tarafani, Wilayani na Mikoani.
2. Wizara hutoa mipango yao kwa Wizara ya Uchumi na Mipango ya Maendeleo.
3. Mazungumzo kati ya Wizara zinazohusika na Wizara ya Uchumi na Mipango ya maendeleo kwa ajili ya ufafanuzi zaidi.

4. Mapendekezo kamili yalipelekwa kwanza na kuzungumzwa na Kamati ya Uchumi ya Baraza la Mawaziri. Mwenyekiti wake ni Rais.
5. Toka hapa mapendekezo yalipelekwa kwenye Kamati ya Taifa ya Utendaji wa TANU.
6. Toka hapa, mapendekezo yalipelekwa kwenye Mkutano wa Mwaka wa TANU kwa ajili ya mazungumzo kwa kirefu.
7. Hatua ya mwisho ilikuwa idhini ya BUNGE, na Rais.

Kutokana na hatua zote hizi, inatudhihirishia kuwa mpango kabla ya kupitishwa, hupitia mazungumzo na majadiliano marefu. Hii inafanywa ili kuhakikisha kuwa mipango yote inapangwa kufuatana na matakwa pamoja na shida za umma. Upangaji wa mpango huu wa Pili wa Miaka Mitano, unakusudiwa kutekeleza kanuni za Azimio la Arusha. Mpango huu una kanuni tano :

I. *Usawa wa hali ya Maisha :* Mpango huu unakusudiwa kugawa faida za maendeleo kwa jamii yote nchini;

II. *Ujamaa :* Mpango unasisitiza uendelezaji wa kazi fulani za uchumi ambazo zinatia moyo juhudi za pamoja bila ya kuwepo na tofauti kubwa za mali na mapato.

III. *Kujitegemea :* Mpango unasisitiza maendeleo kwa njia ya ukusanyaji ya kusanyaji na utumiaji kwa ukamilifu raslimali za nchini hasa kwa kutegemea nguvu za wananchi vijijini.

IV. *Mabadiliko ya uchumi na Maisha ya Watu :* Mpango umesisitiza upanuaji wa haraka wa uwezo wa kutoa mapato ili kutayarisha msingi wa mabadiliko ya nchini na maisha ya wananchi hapo baadaye.

V. *Ushirikiano wa Uchumi katika Afrika :* Mpango unasisitiza upanuaji wa ushirikiano katika mambo ya Uchumi na nchi zingine za Kiafrika.

## MPANGO WENYEWE KWA WIZARA YA KILIMO

Ingawaje baadhi ya Idara za Wizara ya Kilimo zimehamishwa na kupelekwa katika Wizara mpya nyingine lakini hata hivyo tutagusia mpango wote kama ulivyokuwa na kama ulivyo kabla ya kuzihamisha Idara hizo. Maelezo yote haya ni kwa ufupi tu, maana maelezo kamili yaweze kupatikana katika mpango wenyewe wa Serikali. Pia "Ukulima wa Kisasa" ulitoa makala maalum ya Saba Saba 1969 kuhusu mpango huu. Ingefaa kila mmoja wetu ausome kwa ukamilifu. Lakini kwa

kifupi, mpango unatuelezea kuwa; kwa upande wa mazao Serikali imeshauri :

(I) Mazao yanayotarajiwa kuongezwa sana :
Mpunga, Nyama, Mazao ya Maziwa, Ngano, Matunda, Mboga, Chai (mahitaji ya kuongeza ubora wake), Tumbaku (ya mvuke), Pamba, Korosho, Mbegu za Mafuta, Maharagwe (Seed Beans), Soya Beans, Kenaf na Samaki.

(II) Mazao yanayo hitaji ukuzaji mdogo :
Mahindi (vile vile inahitaji kupunguza gharama za utoaji), Mtama (Sorghum na Millete), Ndizi (vitoke) na Sukari.

III. Mazao ambayo masoko yote ni ya kadiri, au hata kupunguka :-

Katani, Kahawa, Pareto na Tumbaku inayokaushwa kwa moto).

Mashamba ya Serikali yatalima baadhi ya mazao hayo. Ni nia ya mpango huu kuanzisha mashamba mapya 29 ambayo kati ya hayo: mawili yatakuwa ya ufugaji wa ng'ombe wa kutoa maziwa: na mashamba mengine 9 yatakuwa kama uwanda wa mifugo.

Uvuvi, misitu na mafunzo navyo vimetiliwa mkazo sana, na tegemeo letu kuwa tutafikia shabaha zetu iwapo tutakuwa na ushirikiano mwema katika utendaji wa kazi hizo zetu. Lakini hii peke yake haitoshi. Ni budi twende pia vijijini tukazungumze na wananchi kuona kama wanaweza kuongeza juhudi zao katika utendaji bora wa kazi za kuutekeleza mpango.


*TUSISAHAU, SOTE TUNAOHUSIKA KWAMBA NI WAJIBU WETU KUUSOMA MPANGO WENYEWE KWA MAKINI NDIPO TUWEZE KUTAMBUA WAJIBU WETU KWA TAIFA.*

Azimio la Arusha linatuambia kuwa sehemu kubwa ya eneo ni lenye rutuba na mvua ya kutosha. Nchi yetu inaweza kutoa mazao ya aina mbali mbali ambayo tunayahitaji kwa chakula na fedha. Mazao ya chakula (na fedha kama tukiyatoa kwa wingi) ni kama vile mahindi, mchele, ngano, maharage n.k. Mazao ya fedha ni kama vile mkonge (ingawa bei yake inapungua) pamba, kahawa, tumbaku, pareto, chai na kadhalika.

Pia nchi yetu ni nzuri sana kwa ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku n.k. Pia twaweza kuvua samaki katika maziwa, bahari na mito.

Wakulima wetu wako katika sehemu ambazo zaweza kutoa mazao haya, kama si yote, walau mawili, matatu au hata zaidi. Kila mkulima wetu aweza kuongeza mazao haya ili ajipatie chakula kingi zaidi, au fedha nyingi zaidi. Na kwa sababu nia kubwa ya maendeleo ni kupata chakula zaidi na fedha zaidi kwa ajili ya kujipatia mahitaji yetu mengine, ndiyo kusema kuwa jitihada ya kuongeza mazao ni jitihada, na kwa kweli ndiyo jitihada peke yake, ambayo italeta maendeleo, yaani chakula zaidi na fedha zaidi kwa wananchi."

Tangu sasa, Wataalam wote wa Kilimo, tutupie macho katika kuitekeleza siasa hii. Viwanda vitakuja, na fedha zitakuja, lakini tukumbuke kuwa msingi wake ni wananchi na juhudi yao na hasa katika KILIMO. "Inawezekana, Timiza Wajibu Wako."



**Mazao ya kila aina yaweza kupatikana nchini mwetu.**

## SEHEMU YA SITA

### Mipango yetu ielekezwe huko Vijijini

## SHABAHA NA MADHUMUNI YA VIJIJI VYA UJAMAA

**SHABAHA :**

Shabaha ya Vijiji vya Ujamaa ni ile ile ya Azimio la Arusha. Shabaha yake ni *Mwanadamu;* yaani kumwezesha kila raia wa Tanzania kuwa na hali nzuri ya maisha.

MAKUSUDI NA MADHUMUNI :

(1) Kuwawezesha wananchi kuunganisha pamoja juhudi zao katika kazi ili waweze kujipatia mapato makubwa zaidi.

Sababu moja kubwa ya umasikini wetu ni kwamba Watanzania hatufanyi kazi vya kutosha. Kuna wanaofanya kazi na kuna wasiofanyakzi kabisa, ingawa wana uwezo wa kufanya kazi.

Wasiofanya kazi licha ya kuitia nchi hasara kwa kutokutoa nguvu zao zifanye kazi, hunyonya nguvu za wenzao wanaofanya kazi. Hivyo hutia hasara mara mbili.

Wanaofanya kazi kosa lao ni kwamba hufanya kazi mmoja mmoja na tena hawafanyi vya kutosha.

Vijiji vya Ujamaa vitasahihisha hayo yote.

(a) Vitakomesha unyonyaji kwa sababu kila mtu atafanya kazi.

(b) Vitawawezesha wananchi kufanya kazi kwa pamoja na kwa muda wa kutosha.

Hayo yatafanya juhudi iongezeke na hali kadhalika mapato.

2. Kuwawezesha wananchi kufanya kazi zao kwa maarifa na kwa kutumia vyombo vya kisasa ili kujipatia mazao mengi na bora zaidi.

*Ujinga* ni sababu moja nyingine ya umasikini wetu. Vijiji vya Ujamaa vitaondoa dosari hii.

(a) Vijiji vya Ujamaa vitawezesha wataalamu kuwafikia wananchi kwa urahisi zaidi, na hata kuweza pia kuhakikisha kuwa wanayofundisha yanatimizwa kweli.

(b) Vijiji vya Ujamaa vitawawezesha wananchi kujipatia utaalamu fulani wa kazi. Hii itafanya watalaamu wawafikie kwa mambo makubwa tu.

(c) Vijiji vya Ujamaa vitawawezesha wananchi kujipatia

vyombo vya kisasa kwa kazi mbali mbali, kama vile za kilimo, ufugaji, na kadhalika.

3. Kuwawezesha wananchi kuwa na mipango katika kazi zao. Sababu nyingine ya umaskini wetu ni "udogo dogo wa shughuli za Uchumi".

Vijiji vya Ujamaa vitaondoa dosari hii. Vitakuwa na mipango ya kazi kwa kila shughuli. Mipango hiyo itakuwa ya kila siku, kila juma, kila mwezi, kila mwaka, hata zaidi. Pia vitaweza kushiriki kwa vizuri zaidi katika kutengeneza mipango ya Maendeleo ya Wilaya, ya Mkoa na hata ya Taifa. Kwa njia hii mipango ya Vijiji itakuwa na uhusiano na mipango ya Wilaya, ya Mkoa na ya Taifa. Kwa kuwa na mipango, kila Kijiji cha Ujamaa :-

(a) Kitaweza kufanya kila kazi kinachotaka ifanywe kwa majira na wakati unaofaa.

(b) Kitaweza kuepukana na hasara zitokanazo na kufanya kazi isiyotakiwa au isiyofaa kwa wakati ule na mahali pale, kwa mfano kupanda mazao yasiyofaa mahali pale au yasiyotakiwa wakati ule.

(c) Kitaweza kujifunza kwa vizuri zaidi matatizo ya shughuli mbali mbali ambazo hazikufanikiwa na kuyatafutia dawa yake.

(d) Kitatumia mipango yake kama mnyampara wa wana kijiji wote hata kumwezesha kila mtu kuua moyo wa ulegevu na badala yake kujenga moyo wa kujitawala binafsi na wa kufanya kazi kwa bidii.

4. (a) Kuwawezesha wana kijiji kugawana kazi kwa kufuata uwezo wa mtu, umuhimu wa kazi, majira ya mwaka, na mahitaji ya kijiji.

Sababu nyingine ya umaskini wetu ni kwamba mkulima kijijini huwa na kazi za aina nyingi mno, yaani yeye huwa kila kitu — huwa mkulima, mfugaji, fundi seremala, mwashi, fundi wa nguo, wa viatu, mganga, wakili, mlinzi, na kadhalika. Hali hii humfanya ajifanyie kazi hizo ovyo ovyo tu.

Isitoshe kwa kukosa utaratibu wa kugawana kazi mara nyingi kazi za maana huachiwa wasiostahili kuzifanya, na wenye kustahili wakajikalia tu, mathalani kilimo na ufugaji badala ya kushughulikiwa na wanaume mahali pengine utakuta wameachiwa wanawake na watoto; wanaume wao kujikalia wakilewa tu.

Vijiji vya Ujamaa vitatoa dosari hii.

(b) Kuwawezesha wananchi kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Kwa sasa wananchi wanavutwa kukimbilia mijini. Vijiji vya Ujamaa vitapunguza sana watu wa kwenda kutafuta kazi mijini. Licha ya kazi za kilimo zitakazopatikana kijijini, kijiji kitaweza vile vile kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Viwanda hivyo vitatoa nafasi ya kazi zaidi kwa wana-kijiji, na kuweza pia kuongeza mapato ya kijiji.

5. Kuwawezesha wananchi kujipatia huduma za lazima kwa maisha kama vile maji, hospitali, shule, maduka, masoko na kadhalika.

Jambo hili litaokoa wakati na nguvu nyingi zinazopotezwa sasa katika kutafuta mahitaji hayo.

6. Kuwawezesha wananchi kuijua na kuielewa siasa ya nchi na kwa njia hiyo kuwafanya wawe huru zaidi.

Siasa ya TANU ni siasa safi. Ni siasa safi kwa kuwa inaamini katika usawa wa binadamu. Na hakuna siasa safi zaidi ya hiyo. Lakini basi bila wananchi wenyewe kuijua siasa hii na kuisimamia haitatimizwa ipasavyo.

Vijiji vya Ujamaa vitawasaidia wananchi waijue barabara siasa hii na kuhakikisha kwamba inatimizwa barabara miongoni mwao. Wakijua siasa hii wataijua kweli, na kuondokana na udanganyifu.

(a) Wataijua kweli kuhusu wao wenyewe — madaraka yao, uwezo wao na mipaka yao.

(b) Wataijua kweli kuhusu viongozi wa TANU na Serikali — madaraka yao, uwezo wao na mipaka yao.

(c) Watajua kweli kuhusu Katiba ya Chama na ya Serikali uwezo wake na mipaka yake.

(d) Wataijua kweli kuhusu siasa ya Ujamaa na Kujitegemea nini maana yake na nini faida yake.

Kujua hayo kutawafungua kutoka katika minyororo ya ujinga na hofu na kuwaondolea kasumba na udanganyifu wa kila aina. Kutawafanya wawe huru kweli, kutawafanya waongeze juhudi katika kazi zao; kutafanya maisha yao yastawi.

7. Kuimarisha na kudumisha demokrasi. Demokrasi ni utawala wa watu wenyewe. Katika demokrasi watu hawatawaliwi; hujitawala wenyewe. Inapowezekana, huwachagua wenzao fulani kuwawakilisha.

Vijiji vya Ujamaa vitawawezesha wananchi kuwa na utawala wa namna ile.

(a) *Utawala wa nyumbani* — Kila mtu atatawala na kuendesha nyumba yake mwenyewe. Hakutakuwepo na kuingiliwa-ingiliwa ovyo bila sheria na kuwavunjia watu heshima zao.

(b) *Utawala wa Kijiji* — Wanakijiji watatawala na kuendesha mambo ya kijiji chao wenyewe. Watachagua viongozi wao wenyewe, halmashauri zao na hata kuwa na mikutano ya kijiji kizima. Mipango na kazi za kijiji zitatengenezwa na kukubaliwa na wana kijiji wenyewe. Viongozi wa TANU na Serikali wajibu wao utakuwa ni kushauri tu.

(c) Katika mabaraza ambayo wana kijiji hawawezi kufika wote, kwa mfano Halmashauri ya Wilaya, Halmashauri za Maendeleo ya Mkoa, Bunge, wananchi watachaguana wenyewe nani wa kwenda katika mabaraza hayo.

(d) Wale watakaochaguliwa kwenda kwenye mabaraza hayo, watakuwa mawakili wa kweli, maana watakuwa wametoka kweli vijijini. Tena kwa kuwa wenyewe ni wa kijiji itakuwa vyepesi kwa wanakijiji wenzao kuwarudisha kwenye mstari wanapoanza kwenda kando.

(e) Demokrasi na Utii ni mapacha. Yaani watu wakisha kukubaliana wote kufanya jambo fulani, huwa lazima wote watii na kutimiza uamuzi huo. Vijiji vya Ujamaa vitawezesha wanakijiji kutimiza siasa hii kwa urahisi zaidi.

8. Kuwapatia wana kijiji hifadhi ya maisha yao :-

Kwa sasa wakulima vijijini daima ni watu wenye wasi wasi kuhusu maisha yao kwa kuwa hawana pato la kutumainiwa ama kwa mwezi ama hata kwa mwaka; hawana akiba benki, hawana hata bima ya aina yo yote. Pato lao hutegemea juhudi yao tu na majira ya mwaka. Wakipatikana na maradhi au mwaka ukiwa mbaya, pato lao huharibika, na maisha yao pamoja na ya jamaa nzima huwa katika mashaka.

Vijiji vya Ujamaa vitawaondolea wasi wasi huo. Vitawapatia hifadhi ya daima na ya kuaminika.

(a) *Ujamaa :* Hii itakuwa ndiyo hifadhi ya kwanza na kubwa. Kijiji cha Ujamaa kitafanya kazi kama ya ukoo. Kama vile mtoto wa mtu ni wa ukoo vile vile, hali kadhalika katika kijiji cha Ujamaa, mtoto atakuwa ni wa kijiji vile vile. Mzazi akifa kijiji kitashika madaraka

ya kumtunza kwa ukamilifu, maana wajibu wa kwanza wa kijiji cha Ujamaa ni usalama wa kijiji. Hii ndiyo hifadhi ya kwanza apatayo mwananchi kwa kuwa katika kijiji cha Ujamaa. *Hupata binadamu wenzake wa kumtunza.*

(b) *Akiba ya Kijiji :* Hii ni hifadhi ya pili. Kila kijiji kitajiwekea fungu maalum akiba kwa wasiojiweza, kwa uzee, na kwa mambo ya dharura.

(c) *Akiba ya binafsi :* Kwa kuwa mapato yatakuwa ya kutosha itawezekana kwa mtu mwenyewe binafsi pia kujiwekea akiba yake.

(d) *Akiba ya Taifa :* Kwa kuwa kijiji kitakuwa ni sehemu ya Taifa, kinapokabiliwa na shida kubwa ambayo chenyewe hakiwezi kuitatua, Taifa litakisaidia, na kwa kuwa wanaishi pamoja msaada huo utawafikia kwa upesi zaidi.

9. *Kuimarisha Ulinzi :* Kuna ulinzi wa aina mbili : wa binafsi na wa Taifa. Vijiji vya Ujamaa vitaimarisha aina zote hizo.

(a) *Ulinzi wa mali na maisha ya binafsi.* Kuishi pamoja mahali pamoja kutarahisisha wana kijiji kulinda mashamba yao, mifugo yao, na mali nyinginezo, hata maisha yao wenyewe kutokana na maadui mbali mbali wadudu, wanyama na hata binadamu wenzao. Vile vile kutarahisisha kuwapa mafunzo zaidi juu ya ulinzi, na inapotokea kuwa hatari inawazidi nguvu, itakuwa rahisi wa Taifa kuwapa msaada.

(b) *Ulinzi wa Taifa.* Ulinzi wa Taifa hautegemei jeshi la ulinzi tu. Unategemea wananchi, *kila mwananchi.* Na ili washiriki barabara katika ulinzi wa Taifa mambo kadha yanahitajiwa.

  (i) Kwanza wananchi hawana budi wawe na cha kulinda.
  (ii) Hawana budi wajue barabara siasa ya nchi yao.
  (iii) Hawana budi wawajue maadui zao — siasa yao na hila zao.
  (iv) Hawana budi wajue kidogo maarifa.
  (v) Hawana budi wajue kidogo maarifa ya ulinzi wa kisiku hizi.

Vijiji vya Ujamaa vitawapa wanakijiji yote hayo. Vitawapa cha kulinda — mali, uhuru na maisha mazuri zaidi kuliko walivyopata kuwanayo. Vitawapa nafasi nzuri ya kujifunza siasa ya nchi, maadui zake na hila zao, na hata kiasi cha kutosha cha maarifa ya ulinzi wa kisasa.

10. Kuwarudishia wananchi utu na heshima yao.

Binadamu huzaliwa uchi kama mnyama. Lakini huwa tofauti sana na mnyama. Huwa tofauti kwa kuwa yeye anayo mambo mawili muhimu ndani yake. Anao uwezo wa aina mbali mbali. Pili anao moyo wa kutoridhika na hali aliyo nayo.

Kwa ajili ya hayo binadamu huweza kujitoa kutoka hali moja ya maisha mpaka hali nyingine nzuri zaidi; yaani kwa lugha ya kawaida, huweza kujiendeleza, na kwa kuwa hayo hayana kikomo. Huendelea kuzaana. Kila anapofikia hali fulani ya maendeleo, ule moyo wa kutoridhika hufanya kazi yake — huikataa ile hali ya maisha kuwa haistahili binadamu. Hapo tena binadamu hutoa uwezo wake ili kujipatia hali iliyo nzuri zaidi.

Kifupi ni kwamba maisha ya binadamu ni ya maendeleo daima kutoka hali moja ya maisha mpaka nyingine nzuri zaidi. Binadamu maisha yake ni safari ya kufikia ukamilifu. Huo ndio utu wake na heshima yake.

## SEHEMU YA SABA

### UMUHIMU WA KUFANYA KAZI, NA UTAMADUNI WAKE

Nchi yetu ambayo imekubali kuwa nchi ya Ujamaa kamili imekubali vile vile kuwa nchi ya wakulima na wafanyakazi. Imekataa tabaka mbili za watu : wale wanaofanyiwa kazi na wale wanaofanya kazi. Nchi yetu imekubali aina moja ya watu yaani WAFANYAKAZI. Hivyo Taifa limechagua kuwa na UTAMADUNI WA KAZI na sio utamaduni wa kufanyiwa kazi.

Nchi yenye utamaduni wa kazi ni Taifa ambalo watu wake hupenda kufanya kazi wakati wowote — yaani saa za kawaida za kazi na saa za baada ya kazi. Mtu mwenye utamaduni wa kazi ni yule ambaye anasikia kuwashwa washwa na wasi wasi akikaa tu dakika kadhaa bila kujishughulisha na kazi yo yote. Mtu mwenye mawazo ya Utamaduni wa kazi, kazi kwake ndiyo maisha na hata akipewa lundo la pesa na watumishi ili akae tu ale akitumikiwa hatakubali kamwe kwa sababu anaona akikaa

tu bila kufanya kazi basi hapo hana maisha tena. Kwake kazi ndiyo maisha na kukaa tu ni kujichimbia kaburi.

**MAANA YA KAZI:**

Kazi ni tendo la kitu au vitu, mtu au watu ambao wametumia maarifa na nguvu za aina fulani katika kuleta mabadiliko ya aina fulani. Mabadiliko yo yote yatokeayo, yawe ya hasara au faida, madogo au makubwa hutokana na kazi iliyosababishwa na kitendo cha mtu au watu, kitu au vitu fulani. Humu duniani kwa kawaida hakuna jambo litokealo bila kusababishwa na kazi ya kitu kingine.

Hivyo basi mabadiliko yo yote tunayotaka yatokee au yawepo ni lazima dhahiri kuwa tunataka tuwe na mamlaka juu ya mazingara yetu, lakini, itabidi mazingara hayo tuyafanyie kazi. Tuzalishe chakula cha kutosha na kujenga ghala za chakula hicho kwa ajili ya siku za shida. Tutengeneze mavazi ya kutosha na kujenga nyumba bora na za kisasa. Yote haya ni kujaribu kutawala mazingira kwa njia ya kufanya kazi. Na utamaduni wa kazi ndio utakaotuwezesha kuleta mabadiliko ya mazingara yetu kwa haraka.

**MWANADAMU — KAMA KIUMBE MFANYAKAZI:**

Mwanadamu ameumbwa kwa ajili ya kufanya kazi. Kazi yenyewe kubwa hasa ni ile ya kuwatumikia wengine. Asili ya kufanya kazi imetokana na Mungu mwenyewe ambaye, kwa kufuata maandiko alifanya kazi kwa siku sita na siku ya saba akapumzika. Yeye anafanya kazi tofauti na binadamu. Anapotamka kazi inatendeka, kwa hiyo tamko lake peke yake linaumba au linatekeleza. Na hivyo kazi huwa imetendeka.

Kwetu sisi binadamu ni tofauti. Tumeagizwa kutoa jasho kila mmoja katika kutimiza mahitaji yetu. Asiyekubali maagizo ya kufanya kazi, basi huyo anakuwa kinyume cha Muumbaji na maumbile.

Mwalimu J. K. Nyerere akijaribu kufafanua jambo hili la mwanadamu kama kiumbe mfanyakazi, katika mazungumzo yake ya 13 Juni, 1967 katika ukumbi wa Ofisi ya Bunge, alisema yafuatayo : -

> "Binadamu na kitu 'Kazi' huwezi kuwatenga. Huwezi kutenga binadamu na kazi; kwamba unaufikiria ubinadamu na maendeleo — hata maendeleo. Kuishi tu — acha habari ya maendeleo kwanza, kwamba binadamu anaishi, na anakua, halafu kitu 'kazi' hamna ! Jitihada hamna !

Ubinadamu na kazi havitengwi. Huwezi kutenga binadamu na kazi. Binadamu anakuja katika dunia hii, na ili apate kuishi, hana budi ashindane na matatizo fulani atakayoyakuta katika Ulimwengu huu... Kuishi kwake kunataka ale. Yeye si jiwe.... Jiwe ukishalitupa linaanguka — basi unalisahau. Lakini binadamu ni lazima ale... Sasa atakulaje ? Hakuna kula bila shughuli. Hakuwezekani. Hata kitoto kidogo lazima kijimudumudu. Kama ni ziwa kilinyonye. Kama kitoto hicho kinashindwa kabisa kunyonya, tutakimiminia maziwa, hata hivyo lazima tutumaini kuwa kitoto hiki kitajimudumudu, mwili wake lazima ufanye shughuli kidogo. Lazima ufanye shughuli kidogo. Lazima tutumainie kwamba angalao yale maziwa yakisha ingia yakatumbukia ndani ya kimwili cha mtoto huyu kitashughulika shughulika, kisiposhughulika anakufa. Lazima afe, na ndiyo maana ya kufa. Tukikuta mwili umekaa umepoa, haushughuliki tena, tunasema amekufa. Hauwezi tena kufanya kazi; siyo kwamba hauwezi tena kufanya kazi bali ndani hamna kazi... Uwezo wa kazi umeondoka, kazi hamna, mtu amekwisha koma kufanya kazi; ndiyo maana ya kufa. "Kazi na maisha ni kitu kile kile. Huwezi ukatofautisha kazi na maisha".

Kutokana na mawazo haya twaweza kuelewa kwa uwazi kabisa kuwa binadamu ni mfanyakazi na amezaliwa aishi kwa kufanya kazi. Bazi tabia na maisha ya mwanadamu ni kufanya kazi, kwa hiyo katika mawazo yaliyo sawa, mwanadamu ameumbwa ili awe na UTAMADUNI WA KAZI.

MWANADAMU + KAZI = MAENDELEO.

Katika maarifa ya kiutamaduni, mwanadamu na kazi ni vitu viwili ambavyo vyatakiwa kuunganishwa ili pawepo kitu cha tatu kiitwacho maendeleo. Mara nyingi tumezungumzia MAENDELEO sana na kusahau kutilia mkazo neno : KAZI. Hata katika mpango wa miaka mitano tunafanya kosa lile lile kwa kutaja "Mpango wa maendeleo ya Miaka Mitano" Badala ya kusema : "MPANGO WA MIAKA MITANO YA KAZI za kuzaa Maendeleo". Huu hasa ni mpango wa kazi ambazo twatarajia kuwa baada ya kuzikamilisha vema kutakuwa na maendeleo. Kwa hiyo maendeleo ni matokeo ya kazi zilizokwisha fanywa.

Kwa yule mtu anayefanya kazi maendeleo yake ni ya aina nyingi. Kwanza ni maendeleo ya mwili. Mwili wa yule mfanya

kazi huwa na afya bora au kwa kawaida huwa mkakamavu. Hata anapotembea anaoyesha kwa uwazi kwa mwili wake hupendeza kwa sababu sio mzito na wala hauna ulegevu. Mfano mzuri ni ule wa ma-askari. *Pili* ni maendeleo katika akili. Akili ya mtu yeyote anayejishughulisha na kazi huendelea kukua na wala kutu haina nafasi ya kuzidhoofisha akili zilizozoea kufanya kazi. *Tatu* ni maendeleo katika tabia na utu. Kufanya kazi wakati wote kunapunguza tabia ya kutenda mabaya na mtu anaendelea zaidi katika kutenda yanayofaa kwa manufaa yake mwenyewe na kwa Taifa lake. *Nne,* maendeleo katika uchumi yanakuwa juu katika muda mfupi kwa sababu walio wengi wanatimiza wajibu wao na kuongeza zaidi juu ya ule wailopewa kutimiza. *Tano,* maendeleo katika mazingara yetu yataongezeka. Na nchi nzima itaonekana kwa uwazi kuwa inafanyiwa kazi na kutunzwa. Sehemu nyingi za ardhi na misitu vitaonekana kuwa katika hali nzuri ipendezayo. Ni dhahiri basi kwamba maendeleo ya aina yo yote yatakiwayo yatapatikana baada ya wananchi walio wengi kuzingatia mawazo ya UTAMADUNI WA KAZI.

**TANU NA UTAMADUNI WA KAZI:**

Tangu mwanzo, TANU ilipokuwa ikipigania uhuru ilielewa umuhimu wa utamaduni wa kazi kwa Taifa jipya. TANU ilipigania uhuru ili wananchi waweze kupata nafasi na hali za kufanya kazi na kula jasho lao bila kunyonywa. TANU ilipenda siku zote wananchi wafanye kazi zao za kujenga nchi wakiwa katika hali ya uhuru na watimize wajibu wao wakijua kwa nini wanafanya hivyo.

Vile vile, tangu mwanzo TANU ilielewa kuwa maendeleo mema na ya haraka yatatokana na kufanya kazi kwa bidii na kwa maarifa ya watu walio huru. Kwa hiyo baada ya Uhuru TANU ilitumia msemo muhimu usemao: "UHURU NA KAZI". Hapa ilikuwa na maana kuwa uhuru wetu ni lazima ulindwe, utunzwe na kukuzwa kwa njia ya kufanya kazi. Uhuru bila kufanya kazi, basi uhuru huo hauna maana yoyote. Matamshi na maelekezo yote ya TANU yamekuwa na yana nia ya kulielekeza Taifa katika utamaduni wa kazi ili kila mmoja awe na moyo na tabia ya kupenda na kufurahia kufanya kazi. Hivyo TANU imekuwa kiongozi wa Utamaduni wa kazi tangu ilipoanzishwa.

**AZIMIO LA ARUSHA NA UTAMADUNI WA KAZI:**

Azimio la Arusha ambalo lina siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, moyo wake ni ule wa kujenga nchi yenye tabia na

utamaduni wa kazi. Katika sehemu ya UJAMAA msingi mmojawapo mkubwa unaotiliwa mkazo ni ule wa kitu kinachoitwa "kazi".

Ili tuelewe mawazo haya ya kazi katika moyo wa siasa yetu ya Ujamaa hatuna budi kuelewa kuwa TANU imetamka wazi kabisa kuwa "TANU ni chama cha wakulima na wafanyakazi." Ni chama cha watu wenye tabia ya kufanya kazi, yaani wenye utamaduni wa kazi.

Pia katika siasa ya Ujamaa imetamkwa wazi kuwa nchi yenye Ujamaa kamili ni nchi ya WAFANYA KAZI. Katika nchi ya Ujamaa kamili mtu hamnyonyi mtu, bali KILA AWEZAYE KUFANYA KAZI, hufanya, na kila mfanyakazi hupata pato la haki kwa kazi aifanyayo. Ili kuzuia unyonyaji, ni budi kila mmoja afanye kazi. Basi katika siasa yote ya Ujamaa moyo wa kufanya kazi umepewa nafasi kubwa.

Hali kadhalika katika Azimio la Arusha kitu kimoja kinachotiliwa mkazo sana ni ile siasa ya kujitegemea; kujitegemea kwa mtu binafsi, kwa kijiji, kwa tarafa, kwa milaya, kwa mkoa na mwisho kwa nchi nzima. Na kujitegemea huko tunakuita, KAZI. Kazi ndio njia tu maalumu ya kujitegemea. Basi katika haya yote tunaweza kuelewa kuwa Azimio la Arusha lina nia ya kutuongoza na kutuelekeza katika njia ya utamaduni wa kazi.

**VIPINGAMIZI VYA UTAMADUNI WA KAZI:**

Katika siasa yote ya TANU tumeona kuwa lengo lake ni kuwaelekeza wananchi katika moyo wa kupenda na kufanya kazi, hata neno 'kazi' limekuwa kama wimbo katika hotuba nyingi za viongozi wa TANU.

Ili tuweze kufanikiwa katika siasa ya 'Utamaduni wa Kazi' hatuna budi kuelewa vipingamizi vinavyoweka vikwazo katika siasa ya utendaji bora wa kazi.

Tatizo la kwanza latokana na historia pamoja na elimu yake. Tangu nyakati za Mwarabu mpaka Ukoloni wa Mwingereza, kazi imefikiriwa kuwa ni kitu cha utumwa. Wakoloni walipendelea kuagiza na kusimamia tu kazi bila wao wenyewe kushiriki pamoja na wafanyakazi. Nasi tulikuwa katika hali hiyo ya kuambukizwa na Ukoloni (mawazo hayo) kuhusu kazi. Bahati nzuri TANU imegundua ubovu huu mapema na kujaribu kutibu ugonjwa huu kwa njia ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Tatizo la pili ni lile la "MAPOKEO" yetu ya zamani. Mara nyingi imetajwa kuwa wanaume walio wengi vijijini na wanawake kadhaa wa mijini bado hawajaingiwa na moyo wa kufanya kazi. Azimio la Arusha likizungumzia ubovu huu lasema : 'Yafaa kujiuzulu wananchi wakulima, hasa wanaume, hufanya kazi kwa saa ngapi kwa juma na miezi mingapi kwa mwaka. Ni wengi mno ambao hawatimizi hata nusu ya wastani wa mfanya kazi wa mshahara."

"Ukweli wenyewe ni kwamba vijijini kina mama hufanya kazi sana. Pengine hutimiza saa 12 au 14 kutwa. Hawana Jumapili, na hawana livu. Kina mama wa vijijini hufanya kazi kuliko mtu mwingine ye yote katika Tanzania. Lakini kina baba wa vijijini (na baadhi ya kina mama wa mijini) nusu ya maisha yao ni livu. Nguvu hivi za mamilioni ya kina baba vijijini na maelfu ya kina mama wa mijini ambazo hivi sasa hazifanyi kazi yo yote ila kupiga soga, kucheza ngoma na kunywa pombe, ni hazina kubwa na yenye manufaa zaidi kwa maendeleo ya nchi yetu kuliko hazina ya mataifa matajiri".

Azimio la Arusha linawaonya viongozi wote wapendao nchi hii kuliingilia tatizo na pingamizi hili na kueneza utamaduni wa kazi kwa wananchi hawa. Basi Azimio lasisitiza : "Tutafanya jambo la faida kubwa kwa nchi yetu kama tukienda vijijini na kuwaambia wananchi kwamba wanayo hazina (nguvu ya kazi) hii na kwamba ni wajibu wao kuitumia kwa faida yao wenyewe na faida ya Taifa letu."

Tatizo la tatu ni lile la mazingara mabaya na ukosefu wa vyombo na ujuzi. Hili ni tatizo ambalo liko, lakini haliwezi kuwa kubwa ikiwa watu wana moyo wa utamaduni wa kazi. Watu wakiwa na moyo wa kazi hata kama kuna mazingara yasiyofaa wanaweza kukaa pamoja na kufikiria jinsi ya kubadilisha mazingara yao labda kama ni mtu mmoja tu, atashindwa kuyabadilisha. Ni hakika wanaweza kufaulu ikiwa wote wana moyo wa utamaduni wa kazi.

Pamoja na jambo hili twahitaji kujenga moyo wa kuvumbua na kubuni vyombo vipya kwa ajili ya utendaji kazi wa haraka zaidi. Tusitosheke kutumia vyombo vile vile mwaka kwa mwaka. Tuwe na mawazo ya kubuni vifaa vipya na vizuri zaidi.

Tatizo lingine ambalo laweza kuharibu mawazo mema ya utamaduni wa kazi ni lile la UKOSEFU WA MIPANGO ya kazi. Baada ya uhuru mawazo ya kuwa na mipango ya kazi

utamaduni wa kazi. Katika sehemu ya UJAMAA msingi mmojawapo mkubwa unaotiliwa mkazo ni ule wa kitu kinachoitwa "kazi".

Ili tuelewe mawazo haya ya kazi katika moyo wa siasa yetu ya Ujamaa hatuna budi kuelewa kuwa TANU imetamka wazi kabisa kuwa "TANU ni chama cha wakulima na wafanyakazi." Ni chama cha watu wenye tabia ya kufanya kazi, yaani wenye utamaduni wa kazi.

Pia katika siasa ya Ujamaa imetamkwa wazi kuwa nchi yenye Ujamaa kamili ni nchi ya WAFANYA KAZI. Katika nchi ya Ujamaa kamili mtu hamnyonyi mtu, bali KILA AWEZAYE KUFANYA KAZI, hufanya, na kila mfanyakazi hupata pato la haki kwa kazi aifanyayo. Ili kuzuia unyonyaji, ni budi kila mmoja afanye kazi. Basi katika siasa yote ya Ujamaa moyo wa kufanya kazi umepewa nafasi kubwa.

Hali kadhalika katika Azimio la Arusha kitu kimoja kinachotiliwa mkazo sana ni ile siasa ya kujitegemea; kujitegemea kwa mtu binafsi, kwa kijiji, kwa tarafa, kwa milaya, kwa mkoa na mwisho kwa nchi nzima. Na kujitegemea huko tunakuita, KAZI. Kazi ndio njia tu maalumu ya kujitegemea. Basi katika haya yote tunaweza kuelewa kuwa Azimio la Arusha lina nia ya kutuongoza na kutuelekeza katika njia ya utamaduni wa kazi.

**VIPINGAMIZI VYA UTAMADUNI WA KAZI:**

Katika siasa yote ya TANU tumeona kuwa lengo lake ni kuwaelekeza wananchi katika moyo wa kupenda na kufanya kazi, hata neno 'kazi' limekuwa kama wimbo katika hotuba nyingi za viongozi wa TANU.

Ili tuweze kufanikiwa katika siasa ya 'Utamaduni wa Kazi' hatuna budi kuelewa vipingamizi vinavyoweka vikwazo katika siasa ya utendaji bora wa kazi.

Tatizo la kwanza latokana na historia pamoja na elimu yake. Tangu nyakati za Mwarabu mpaka Ukoloni wa Mwingereza, kazi imefikiriwa kuwa ni kitu cha utumwa. Wakoloni walipendelea kuagiza na kusimamia tu kazi bila wao wenyewe kushiriki pamoja na wafanyakazi. Nasi tulikuwa katika hali hiyo ya kuambukizwa na Ukoloni (mawazo hayo) kuhusu kazi. Bahati nzuri TANU imegundua ubovu huu mapema na kujaribu kutibu ugonjwa huu kwa njia ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Tatizo la pili ni lile la "MAPOKEO" yetu ya zamani. Mara nyingi imetajwa kuwa wanaume walio wengi vijijini na wanawake kadhaa wa mijini bado hawajaingiwa na moyo wa kufanya kazi. Azimio la Arusha likizungumzia ubovu huu lasema : 'Yafaa kujiuzulu wananchi wakulima, hasa wanaume, hufanya kazi kwa saa ngapi kwa juma na miezi mingapi kwa mwaka. Ni wengi mno ambao hawatimizi hata nusu ya wastani wa mfanya kazi wa mshahara."

"Ukweli wenyewe ni kwamba vijijini kina mama hufanya kazi sana. Pengine hutimiza saa 12 au 14 kutwa. Hawana Jumapili, na hawana livu. Kina mama wa vijijini hufanya kazi kuliko mtu mwingine ye yote katika Tanzania. Lakini kina baba wa vijijini (na baadhi ya kina mama wa mijini) nusu ya maisha yao ni livu. Nguvu hivi za mamilioni ya kina baba vijijini na maelfu ya kina mama wa mijini ambazo hivi sasa hazifanyi kazi yo yote ila kupiga soga, kucheza ngoma na kunywa pombe, ni hazina kubwa na yenye manufaa zaidi kwa maendeleo ya nchi yetu kuliko hazina ya mataifa matajiri".

Azimio la Arusha linawaonya viongozi wote wapendao nchi hii kuliingilia tatizo na pingamizi hili na kueneza utamaduni wa kazi kwa wananchi hawa. Basi Azimio lasisitiza : "Tutafanya jambo la faida kubwa kwa nchi yetu kama tukienda vijijini na kuwaambia wananchi kwamba wanayo hazina (nguvu ya kazi) hii na kwamba ni wajibu wao kuitumia kwa faida yao wenyewe na faida ya Taifa letu."

Tatizo la tatu ni lile la mazingara mabaya na ukosefu wa vyombo na ujuzi. Hili ni tatizo ambalo liko, lakini haliwezi kuwa kubwa ikiwa watu wana moyo wa utamaduni wa kazi. Watu wakiwa na moyo wa kazi hata kama kuna mazingara yasiyofaa wanaweza kukaa pamoja na kufikiria jinsi ya kubadilisha mazingara yao labda kama ni mtu mmoja tu, atashindwa kuyabadilisha. Ni hakika wanaweza kufaulu ikiwa wote wana moyo wa utamaduni wa kazi.

Pamoja na jambo hili twahitaji kujenga moyo wa kuvumbua na kubuni vyombo vipya kwa ajili ya utendaji kazi wa haraka zaidi. Tusitosheke kutumia vyombo vile vile mwaka kwa mwaka. Tuwe na mawazo ya kubuni vifaa vipya na vizuri zaidi.

Tatizo lingine ambalo laweza kuharibu mawazo mema ya utamaduni wa kazi ni lile la UKOSEFU WA MIPANGO ya kazi. Baada ya uhuru mawazo ya kuwa na mipango ya kazi

kwa ajili ya Taifa yametiliwa mkazo sana. Jambo ambalo halikumbukwi vya kutosha ni kwamba mipango ya kazi kwa wale wazalishaji mali, yaani wananchi, haikutiliwa mkazo.

Ili wananchi waendelee katika kazi zao za kawaida wanahitaji wazoezwe kuwa na mipango ya kazi zao za kila siku, kila mwezi na kila mwaka. Wananchi, katika mawazo ya utamaduni wa kazi, wazoezwe namna ya kutumia kila dakika walivyo nayo mokononi mwao. Mkulima wa kisasa anayependa maendeleo anaweza kufanikiwa ikiwa anashirikiana na wengine, ikiwa anashirikiana na wengine, ikiwa ana juhudi na anatumia maarifa ya kisasa na pia ikiwa anaweza kupanga kazi zake vizuri na kuwa na rekodi maalumu za kazi.

Tatizo lingine ambalo hatuna budi kulifikiria ni lile la UKOSEFU WA USHIRIKIANO kamili katika shughuli za kiuchumi. Hata kama tutakuwa tumepata mwamko wa utamaduni wa kazi inatupasa kuelewa kuwa mtu mmoja ni vigumu kumudu kazi kubwa zilizo muhimu peke yake. Hapa ndipo ushirikiano unapotakikana. Hii ndiyo sababu siasa yetu inatilia mkazo mpango wa VIJIJI VYA UJAMAA ili wananchi waweze kuishi pamoja kwa ajili ya KUFANYA KAZI PAMOJA KWA FAIDA YAO WENYEWE. Kwa njia ya vijiji vya Ujamaa wananchi wataweza kumudu mambo makubwa zaidi kiutamaduni na kiuchumi.

Viongozi katika idara na mashirika mbali mbali yaendeshayo shughuli za utamaduni vijijini, mijini, mashuleni na vyuoni wana wajibu mkubwa wa kueneza mawazo ya utamaduni wa kazi. Viongozi wenyewe wapate kwanza moyo wa utamaduni wa kazi na waonyeshe mfano kwa wananchi.

"INAWEZEKANA, TIMIZA WAJIBU WAKO".

*Baadhi ya maneno yaliyotumika humu ya Kisiasa na maana zake.*

UJAMAA : Ni mtindo wa maisha ambao msingi wake mkubwa ni Imani katika USAWA wa Binadamu. Mtindo huu ni kinyume cha mtindo wa unyonyaji.

UNYONYAJI : Ni mtindo wa maisha unaomwezesha mtu au kikundi cha watu au tabaka fulani la watu, kupata riziki bila ya wao au yeye kufanya kazi. Yeye au wao, hutegemea mtu au watu wengine kwa kuifanya kazi hiyo.

UBEPARI : Huu ni mtindo wa maisha unao wezesha watu wachache wamiliki njia kuu za kuzalishia mali, kama viwanda, migodi, nguvu za umeme, njia za kusafirishia biashara kubwa za nje na ndani, njia za simu n.k. na kuwatumia wananchi kuzalishia mali kwa faida ya wenye mali wenzao kama vyombo tu vingine vya yaani mabepari.

UKABAILA : Mtindo wa maisha unao wawezesha watu wachache kumiliki ardhi yote, viwanda au majumba na kutumia ardhi hiyo, viwanja hivyo au majumba hayo kwa kukodisha kwa watu wengine ili ajipatie ridhiki bila yeye au wao — kutofanya kazi.


UKUPE : Ni hali ya kuishi na kupata ridhiki bila ya kufanya kazi; kama unyang'anyi, umalaya n.k.

| | |
|---|---|
| DEMOKRASI : | Ni utawala wa watu kwa manufaa ya wote. |
| KABWELA : | Ni neno lililokuwa likitumika mara tu baada ya Uhuru likimaanisha — Wananchi wa hali ya chini. |
| NAIZA : | Ni neno lililotokana na neno la Kiingereza "Africanisation". Neno hili lilitokea mara tu baada ya Uhuru wakati Waafrika waliposhika nafasi za Wazungu. Baada ya wananchi kushindwa kutamka neno hilo refu, walifupisha na kuita "NAIZA" yaani mtu mwenye madaraka makubwa. |
| UMMA : | Wananchi wote kwa ujumla, yaani wakulima na wafanyakazi. |
| KUJITEGEMEA : | Kujitegemea kwa nchi maana yake ni kwamba nchi inajiendeleza yenyewe kwa kutegemea raslimali yake, juhudi na uwezo wa wananchi wake bila ya kuombaomba misaada mingi toka nchi ya kigeni. Msingi wake mkuu ni KUJIAMINI. |

Soma maelezo zaidi kutokana na vitabu hivi :-

UJAMAA — Mwl. J. K. Nyerere.
Kupanga ni Kuchagua — Mwl. J. K. Nyerere.
Uhuru na Maendeleo — Mwl. J. K. Nyerere.
Freedom and Unity — Mwl. J. K. Nyerere.
Freedom and Socialism — Mwl. J. K. Nyerere.
Ijue TANU — Makao Makuu ya TANU.
Katiba ya TANU — Makao Makuu ya TANU.
Mpango wa Pili wa Miaka Mitano wa Maendeleo.

SPE
S494
.S.A7
S5
copy 2




**Soma MWONGOZO mpya wa TANU 1971 na uuelewe vizuri sana**

KIMEPIGWA CHAPA NA NATIONAL PRINTING CO. LTD. DSM.